TOFAUTI YA MSAMIATI WA LAHAJA YA KIPEMBA CHA KASKAZINI NA KIPEMBA CHA KUSINI

SITI FAKI ALI

TASINIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2015

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu yenye mada *"**Tofauti za Msamiati Wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini,*** na nimeridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa Shahada ya Uzamili ya Isimu kwa Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

…….

Dkt. Zelda Elisifa

(Msimamizi)

……

Tarehe

HAKIMILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, Kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Siti Faki Ali** natamka na kuthibitisha kuwa Tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Digrii ya aina yeyote ile.

……

Saini

……

Tarehe

TABARUKU

Kazi yangu hii naitabaruku kwa familia yangu yote hasa mama yangu mzazi , Bibi Hidaya Omar Hassan iwe ni ukumbusho wake kwa malezi bora alonilea na kunipatia Elimu.

SHUKURANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu (S.W) kwa kunijaalia afya njema na uwezo wa kupata fursa ya kujiunga na masomo ya Digirii ya M A Kiswahili kwa mwaka wa masomo 2014/2015 kwani wengi hawakubahatika kupata fursa hiyo.

Pili, shukurani zangu za dhati zimwendee msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Zelda Elisifa kwa kunisimamia kazi hii mpaka ikakamilika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa taufiki ya kuniongoza mpaka ikamaliza kazi sina cha kumlipa ila namuomba Mwenyezi mungu amjaalie kila la kheri hapa duniani na kesho akhera.

Napenda pia kuishukuru familia yangu yote kwa kuniunga mkono kwa hali na mali wakati wote nikiwa masomoni hasa kwa baba na mama yangu mzazi kwa kunipa msingi bora wa Elimu hadi kufikia ngazi hii ya umahiri zaidi.

Shukurani pia zimwendee mume wangu Bwana Bakar Omar Khatib kwa msaada wake mkubwa wa hali na mali na ruhusa kama mke katika ndoa wakati wa kipindi chote cha masomo yangu na jinsi alivyostahamili na ulezi wa familia bila kujali upweke katika kipindi chote cha masomo.

Shukurani zangu za dhati pia ziende kwa familia yangu yote hasa kwa wazazi wangu, baba yangu Bwana Faki Ali Hamad na mama yangu Bibi Hidaya Omar Hassan kwa malezi bora walonilea na kunipatia Elimu. Pia kwa watoto wangu wapendwa Rayyan, Omar, Abdul-Basit na Sharmin. Kwa uvumilivu wao ,namuomba Mwenyezi Mungu awape maisha mema ya duniani na kesho akhera.

Shukurani zangu za pekee ziende kwa mwalimu Bakar Kombo Bakar ambae ni muendeshaji wa ngazi hii kwa tawi la Pemba kwa mchango wake mkubwa alionipatia katika masomo yangu. Hakusita kunihimiza na kuniongoza kila wakati ili niweze kukamilisha kazi hii kwa wakati. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie kila lenye kheri na mafanikio mema ya hapa duniani na kesho akhera.

Shukurani nyengine ziwaendee wahadhiri, wakufunzi, wahudumu na wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa mchango wao mkubwa katika kusukuma mbele gurudumu la masomo kwa ujumla.

Aidha, natoa shukurani kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kunipa ruhusa ya kujiunga na masomo ya ngazi hii. Pia shukurani ziwaendee wanafunzi wenzangu kwa ushirikiano wao mkubwa katika masomo hadi kukamilisha kazi hii.

Nitakuwa mwizi wa fadhila nisipotoa shukurani zangu za dhati kwa uongozi wa skuli yangu ya Chasasa na watoa taarifa ya utafiti katika vijiji vya Micheweni, Kiuyu, Maziwang’ombe, Kangani, Chokocho na Mwambe.kwa ushirikiano wao mkubwa katika kufanikisha kazi hii.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini ikiwa ni hatua mojawapo ya kuitafiti lugha ya Kiswahili na lahaja zake ambapo kazi hii inatoa mawazo ya awali katika kuelezea tofauti za msamiati wa Kipemba kinachozungumzwa katika maeneo hayo. Data ya uwandani ya utafiti huu umekusanywa kwa kutumia mbinu za dodoso, mahojiano na ushuhudiaji ambapo sampuli-tegemea fursa na sampuli eneo zimetumika kuchagua watoa taarifa kwa vigezo vya umri, elimu na ukazi. Nadharia ya isimulinganishi, orodha ya Swadesh na mbinu za uchambuzi matini zimetumika kuchambua data hiyo. Katika kipengele cha msamiati ambacho kimechunguzwa, Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa kuna tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Hivyo, Kipemba cha Kaskazini kinaonekana kuhifadhi msamiati Kipemba cha kale (lahaja) ambapo Kipemba cha Kusini kinataka kufanana na Kitumbatu lakini kwa kiasi kikubwa kinaelekea kwenye usanifu. Kwa vile, utafiti huu unabainisha kuwa kuna tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini, utafiti huu hauhitaji hitimisho la haraka. Uchunguzi zaidi unahitajika kuchunguza asili ya watu na chimbuko la lahaja katika maeneo hayo.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO LA MTAHINIWA ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **viii**

MAJEDWALI ..... **xiii**

VIAMBATISHO ..... **xiv**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI **1**

1.1 Utangulizi 1

1.2 Msimbo wa Tatizo la Utafiti 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.4 Malengo ya Utafiti 4

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti 4

1.4.2 Malengo Mahususi 4

1.5 Maswali ya Utafiti 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti 5

1.7 Upeo wa Mada 6

1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake 6

1.9 Muhutasari 6

SURA YA PILI **8**

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI 8

2.1 Utangulizi 8

2.2 Utafiti wa Lahaja Ulaya na Marekani 8

2.3 Utafiti wa Lahaja Barani Afrika 9

2.4 Utafiti wa Lahaja za Kiswahili 10

2.5 Kiunzi cha Nadharia 15

2.6 Muhutasari 16

SURA YA TATU 17

MBINU ZA UTAFITI 17

3.1 Utangulizi 17

3.2 Muundo wa Utafiti ..... **Error! Bookmark not defined.**

3.3 Eneo la Utafiti 17

3.4 Walengwa wa Utafiti (Usampulishaji) 18

3.5 Sampuli ya Watafitiwa 19

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 20

3.6.1 Mbinu ya Dodoso 20

3.6.2 Mbinu ya Mahojiano 21

3.6.3 Mbinu ya Ushuhudiaji 21

3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data 22

3.8 Uwasilishaji wa Data 23

3.9 Maadili ya Utafiti 23

3.10 Muhutasari 24

SURA YA NNE 25

UWASILISHAJI WA DATA 25

4.1 Utangulizi 25

4.2 Msamiati wa Kipemba 25

4.2.1 Kutofanywa Utafiti wa Kina 26

4.2.2 Kipemba Kutokuwa na Msamiati Mmoja 26

4.2.3 Ukosefu wa Vyanzo vya Data 27

4.2.4 Ukosefu wa Maelezo ya Kina 27

4.3 Tofauti za Kimatamshi 28

4.3.1 Tofauti za Mpishano wa Sauti 28

4.3.2 Mpishano wa Konsonanti 29

4.3.3 Mpishano wa Irabu 30

4.3.4 Mpishano wa Nusu Irabu 30

4.3.5 Udondoshaji wa Sauti 31

4.3.6 Tofauti za Ukakaishaji wa Sauti 32

4.3.7 Tofauti za Lafudhi 33

4.3.8 Tofauti za Matumizi ya Mpumuo 34

4.3.9 Utokeaji wa Kibinuaulimi [nd^{r}] 35

4.4 Tofauti za Kileksika (Maumbo) 36

4.4.1 Tofauti za Leksika 37

4.4.2 Tofauti za Kimofolojia kwa Baadhi ya Maneno 37

4.5 Sababu za Tofauti za Msamiati 38

4.5.1 Umbali wa Maeneo Kijiografia 39

4.5.2 Sababu za Kihistoria 40

4.5.3 Kutawanyika kwa Watu 41

4.5.4 Shughuli za Kiuchumi 42

4.5.5 Mwingiliano na Jamiilugha Nyingine 44

4.6 Muhutasari wa Sura 45

SURA YA TANO 47

MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 47

5.1 Utangulizi 47

5.2 Muhutasari wa Mjadala wa Utafiti 47

5.2.1 Muhutasari wa Jumla 47

5.2.2 Muhutasari wa Ugunduzi 48

5.3 Hitimisho 49

5.4 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti Zaidi 50

MAREJELEO 51

VIAMBATISHO 55

MAJEDWALI

Jedwali Na. 4.1: Mpishano wa Konsonanti 29

Jedwali Na. 4.2: Mpishano wa Irabu 30

Jedwali Na. 4.3: Mpishano wa Nusu-Irabu 31

Jedwali Na. 4.4: Udondoshaji wa Sauti 31

Jedwali Na. 4.5: Ukakaishaji wa Sauti 32

Jedwali Na. 4.6: Tofauti za Lafudhi 34

Jedwali Na. 4.7: Matumizi ya Mpumuo 35

Jedwali Na. 4.8: Matumizi ya Kibinua ulimi 36

Jedwali Na. 4.9: Tofauti za Kileksika 37

Jedwali Na. 4.10: Tofauti za Kimofolojia 38

Jedwali Na. 4.11: Sababu za Mwachano wa Kijiografia 39

Jedwali Na. 4.12: Sababu za Kihistoria 41

Jedwali Na. 4.13: Mtawanyiko wa Watu 42

Jedwali Na. 4.14: Sababu za Kiuchumi 43

Jedwali Na. 4.15: Sababu za Mwingiliano 44

VIAMBATISHO

Kiambatishi I: Dodoso la Kuchunguza Tofauti ya Msamiati..... 55

Kiambatishi II: Mwongozo wa Maswali ya Hojaji 60

Kiambatishi III: Orodha ya Msamiati Uliobainishwa na Watafitiwa kwa Kutumia Dodoso……63

Kiambatishi IV: Orodha ya Msamiati Uliotafitiwa..... 64

Kiambatishi V: Matini Mbalimbali 69

Kiambatishi VI: Barua ya Ruhusa ya Utafiti 73

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza vipengele vinavyotoa taarifa za utafiti kama vile msimbo wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, upeo wa mada, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo na mwisho ni muhutasari wa sura hii.

1.2 Msimbo wa Tatizo la Utafiti

Dhana ya lahaja imefasiliwa na wataalamu tofauti wa zama za nyuma hadi sasa ambayo imekuwa ikitajwa sambamba na dhana ya lugha. Kwa mfano, Stigand (1915) katika utafiti wake alibaini kuwa lahaja ni mabadiliko ya sauti na msamiati baina ya lahaja mbalimbali. Yeye anazichukulia tofauti za kifonolojia na kimsamiati baina ya lugha zinazokaribiana kimatamshi kuwa ndio lahaja.

Wasemaji wa lugha moja wanaweza kutofautiana kiusemaji kulingana na maeneo walikosambaa. Kwani huu ndio msingi wa lahaja ambapo huakisi tofauti za lugha zinazojitokeza miongoni mwa wazungumzaji wa lugha moja wanapoachana kijiografia. Wazungumzaji hao wanaweza kutofautiana kimatamshi na pia katika baadhi ya msamiati na hata kimaana. Katika lugha ya Kiswahili tofauti hizo zinadhihirika katika lahaja zake. Massamba (2004) anaeleza kuwa lahaja ni lugha maja wapo baina ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo kama lafudhi au msamiati usio wa msingi.

Fasili hiyo ya lahaja inadhihirisha wazi kuwa tofauti kama hizo zipo katika maeneo mengi kunakozungumzwa Kiswahili kwani tofauti za wazi baina ya lahaja za Kiswahili katika maeneo zinajidhihirisha katika vipengele vya kifonolojia,kimsamiati,kimofolojia,kimuundo na hata kimaana.

Wataalamu wengi wa lugha ya Kiswahili kama vile kipacha (2003), Masebo na Nyangwine (2002), Kitiso (1988), Bakari (1988) wanaeleza kuwa Kipemba ni lahaja inayotumika katika kisiwa cha Pemba kana kwamba kuna usawa wa watumiaji wote wa lahaja hii. Baadhi ya wataalamu waliotafiti lahaja katika kisiwa cha Pemba kama vile, Whiteley (1958), Polome (1967), Khamis (1984), Maganga (1991), Nurse na Hinnebusch (1993) na Massamba (2006) wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili inayozungumzwa kisiwani Pemba inatofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Ukweli ni kuwa Wapemba wanaoishi eneo la Kaskazini na wale wa Kusini wanatofautiana kimsamiati katika lahaja hii kwa kiwango ambacho tungediriki kusema ni lahaja mbili tofauti.

Wataalamu kama vile Whitely (1958), Polome (1967) na Khamis (1984) ni miongoni mwa watafiti waliojaribu kuchunguza lahaja za Kiswahili za kisiwa cha Pemba. Wataalamu hawa wanabainisha kuwa Kiswahili kizungumzwacho Pemba kinatofautiana kimatamshi na baadhi ya msamiati kutoka eneo moja hadi jingine. Pia Kipacha (2003:132-133) anaorodhesha leksimu za Pemba. Kwa kuthibitisha hilo Massamba (2007:71) anafafanua:

> “Ukienda Pemba kwa mfano Kiswahili kinachozungumzwa Micheweni ni tofauti na kile kinachozungumzwa katika kisiwa cha Kojani.

Licha ya baadhi ya wataalamu kueleza tofauti za lahaja ya kisiwa cha Pemba na kutoa mifano michache kwa mujibu wa uelewa wa mtafiti hakuna utafiti uliofanywa kwa madhumuni ya kubainisha tofauti ya msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha kusini.Jambo ambalo limekuwa ombo la kitaalamu.Kwa kuangalia tafiti hizo tunaweza kubaini kuwa hazikuchunguza tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha kaskazini na Kusini. , hivyo mtafiti amebaini kuwa kuna ombo la maarifa kuhusu tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Hata utafiti wa Khamis (1984) ambao uligusia tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba cha mijini na Kipemba cha vijijini, nao unakabiliwa na pengo la wakati kwani ni zaidi ya miaka 30 sasa tokea kufanyika kwa utafiti huu ambapo kuna mabadiliko makubwa ya msamiati .

Hivyo Utafiti huu ulichukuza tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. TUKI(1981) Kwa upande wake inafasili msamiati kuwa ni jumla ya maneno yanayotumiwa na watu katika lugha

1.3 Tatizo la Utafiti

. Stigand (1915) alitafiti msamiati wa Kipemba ulivyofanana au kutofautiana na lahaja nyengine za Kiswahili.Na kugundua kuwa Kipemba kinafanana na kutofautiana na lahaja nyengine za Kiswahili.katika maelezo yake anaeleza kuwa “Kipemba ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba.Inafanana sana na

lahaja ya zamani, ina maneno mengi yaliyochukuliwa kutoka wakaazi wa zamani wa visiwani”.

Khamis (1984) alichunguza tofauti baina ya Kipemba kizungumzwacho mjini na kile cha vijijini.Aligundua kwamba Kiswahili kizungumzwacho katika maeneo ya vijijini kinatofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka eneo moja hadi jingine.

Juma (2011) alitafiti tofauti za kiisimu baina ya Kiswahili cha micheweni na Wete katika kisiwa cha Pemba.Katika utafiti wake aliangalia tofauti za kifonolojia,kimsamiati,kimofolojia.Katika kipengele cha msamiati aligundua maneno yenye maana au maana zinazokaribia na yanavyotofautiana kimaumbo na kubainisha tofauti za msamiati kupitia vikoa vya maana.

Mtafiti katika utafiti huu alitafiti,Tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.

.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza tofauti ya msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.

1.4.2 Malengo Mahususi

Katika kufikia lengo kuu, malengo mawili mahsusi yameongoza utafiti huu; nayo ni:

(a) Kubainisha tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.

(b) Kueleza sababu zilizopelekea tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umejaribu kujibu maswali yafuatayo:

(a) Kuna tofauti gani za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini?

(b) Ni sababu zipi zilizopelekea utofauti wa msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa katika historia ya mgawanyo wa lahaja na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Umuhimu wa utafiti huu unajibainisha katika nyanja kuu tatu kama ifuatavyo:

(a) Utafiti huu utakuwa ni utajirisho wa matini za kiisimu katika kubaini tofauti za msamiati wa lahaja ya Pemba Kimkoa.

(b) Utafiti huu utakuwa ni msaada kwa wanafunzi, wanaisimu, wasomi wa dailektolojia na watafiti katika kutafiti lahaja za Kiswahili.

(c) Utafiti huu utawasaidia wazungumzaji wa Kiswahili waishio Pemba kufahamu tofauti ya misamiati iliyomo katika lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini.

1.7 Upeo wa Mada

Kimsingi utafiti huu umechunguza tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Kwa hivyo, haukujiingiza katika maswala ya fonolojia, mofolojia na miundo kwa sababu kuchambua vipengele hivyo si lengo la utafiti huu. Hasa ikizingatiwa ufinyu wa muda uliopangwa kufanya utafiti. Vipengele hivyo vinaweza kujadiliwa katika tafiti zijazo. Hata hivyo, hatuwezi kusema kuwa vipengele hivyo havikutajwa kabisa, bali vimeweza kubainishwa ili kutoa ufafanuzi katika utafiti huu pale ilipobidi.

1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Wakati mchakato wa utafiti huu ukiwa unaendelea mtafiti alikabiliwa na vikwazo vifutavyo:-

(i) Tatizo katika ukusanyaji wa data, maneno yaliweza kuleta ugumu wa uelewa kwa vile mtafiti alikuwa haelewi vyema msamiati wa eneo linalohusika. Mtafiti alitafuta watu wenye uelewa wa msamiati wa eneo hilo na Kiswahili sanifu kwa lengo la kufafanua.

(ii) Tatizo katika mbinu ya mahojiano, wakati mwingine iliwafanya wahojiwa kuingiza hisia zao na mitazamo binafsi. Hata hivyo, ili kuzuia data zisiathirike kiuhalisia, mtafiti aliandaa maswali elekezi yaliyo mwezesha kupata data inayokidhi madhumuni ya utafiti huu.

1.9 Muhutasari

Katika sura hii tumeeleza vipengele vinavyotoa taarifa za utafiti kama vile jiografia ya mahali pa utafiti, msimbo wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti na maswali ya utafiti.

Pia, tumebainisha umuhimu wa utafiti, upeo wa mada, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo na mwisho ni muhutasari wa sura hii.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha na kuelezea mapitio ya kazi tangulizi. Katika kueleza mapitio ambayo yametumika katika utafiti huu tumeelezea tafiti za lahaja ulaya na Marekani, Afrika na Utafiti wa lahaja za Kiswahili. Pia sura hii inaelezea kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu na mwisho ni muhutasari wa sura.

2.2 Utafiti wa Lahaja Ulaya na Marekani

Watafiti wengi ulimwenguni wametafiti lahaja za lugha mbali mbali na kubaini kuwa kuna kufanana ama kutofautiana kwa lahaja hizo katika vigezo vya kiisimu. Ash na Boberg (2006:53-54) wanaeleza kwamba wasemaji wa Marekani Kusini huonesha tofauti katika maeneo yao kwa kutumia ‘diphthong’ katika maneno hayo. Tofauti hasa ni Carolina Kaskazini, Kusini na Magharibi ambako irabu unganifu /ai/ hutamkwa kama irabu moja /a/ ambapo wasemaji wengi huonesha kipengele hiki katika ncha ya maneno na kabla ya konsonanti alionesha lakini si kabla ya konsonanti isompumuo.

Kortman (2003) analinganisha maumbo ya maneno na sentensi katika lahaja za Kiingereza. Katika utafiti wake aligundua kuwa katika Magharibi ya Uingereza ambayo ina makala kadhaa za kisarufi ambazo ni tofauti na Visiwa vya Uingereza. Kwa mfano anasema, “Mfumo wa kisemantiki, majina yanaangaliwa jinsia katika makundi na majina yanayohesabika ambapo tofauti zipo kati ya vitu vyenye uhai na visivyo uhai na kwa binaadamu na asiekuwa binaadamu ambapo huchukua ‘she’ na

‘he’ ambapo ‘she’ hutumika kuashiria binaadamu wa kike na ‘he’ wa kiume au kwa vyote na ndipo ilipoonekana tofauti. Alieleza pia si lahaja ya Uingereza lakini pia katika Scotland, Ireland ya Kaskazini na Jamuhuri ya Ireland kitenzi katika wakati uliopo huchukua –s mwishoni na vilevile mtu wa tatu umoja mwishoni huchukua –s katika Kiingereza sanifu kwa maneno mengine.

Prasad (2012) alifanya utafiti katika lugha za Kichina alibaini kwamba watu wa china wa eneo moja wanazungumza tofauti na eneo jingine na kati yao hakuna mfanano wa aina yeyote. Kwa mfano katika lahaja ya Cantonese inayozungumzwa na watu wa Canton, Pekingese inayozungumzwa na watu wa Peking na Yunnanese inayozungumzwa na watu wa Yunani. Licha ya kwamba lahaja zote hizi zinapatikana katika jamii moja na kuonesha mfanano lakini tofauti zipo kati yao.

2.3 Utafiti wa Lahaja Barani Afrika

Gesare (1992) alishughulikia Mofolojia ya Lugha ya Ekegusii. Ametumia nadharia ya Umiundo kuafikia malengo ya kazi yake. Katika kuchambua majina ya lugha ya Ekegusii alisema ni aina moja katika maumbo ya lugha. Pia alieleza vipengele kadhaa kama vile toni katika lugha ya Ekegusii na uainishaji wa nomino za ngeli, ambavyo vitatusaidia katika utafiti wetu.

Nyandabo (2013) alishughulikia uchanganuzi linganishi wa sintaksia ya sentensi sharti za Kiswahili sanifu na Ekegusii. Katika kazi yake alieleza miundo ya sentensi na vipashio vya masharti . Ingawa kazi yake ilikuwa ya kisintaksia lakini itatusaidia katika utafiti huu ikikumbukwa kuwa maneno ndio yanayounda sentensi.

2.4 Utafiti wa Lahaja za Kiswahili

Mnamo karne ya 20 walijitokeza wataalamu wa kigeni kutafiti baadhi ya lahaja za maeneo mbali mbali (lahaja za Kiswahili). Miongoni mwa lahaja zilizotafitiwa ni kimtanga'ta (Whiteley, 1956), Kivumba (Lambert, 1957), Chichifundi (Lambert, 1958), Kijomvu na Kingare (Lambert, 1958) na Kipemba (Whiteley, 1958). Pia mwishoni mwa karne hiyo waliibuka wasomi wazawa wakachangia juhudi zilizofanywa na wageni za kutafiti lahaja za Kiswahili. Baadhi yao ni Temu (1980), Batibo (1982), Khamis (1984), Mshindo (1989) na Maganga (1991). Lakini wengi wa wataalamu hawa wanajikita katika kutafiti vipengele vya sarufi za lahaja hizo kwa kuvilinganisha na vile vya Kiswahili Sanifu badala ya kulinganisha na kutofautisha usemaji wa eneo moja na jengine. Kuhusu lahaja ya Kipemba Sacleux (1909:1) anaeleza kuwa Kipemba kina lahaja ndogo nne (4) na kuzitaja kama ifuatavyo.

> "Kipemba cha Kusini, kipemba cha kivitongoji Mvumoni, Ki-Chake Chake cha Chake Chake na Kimsuka cha Chaleni"

Katika kazi yake hiyo anaeleza matumizi ya kiambishi "ki-" kinachotumika katika Kipemba badala ya "ch-". Mfano "kyombo kyema" badala ya "chombo chema". Hata hivyo, kazi yake ina walakini kwani haibainishi kwa kina tofauti za kiisimu za lahaja hizo. Kwa upande wa mgao wa lahaja, pia lahaja zote alizotaja zipo Kusini isipokuwa Kimsuka cha Chaleni. Utafiti wake haukuonesha tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba.

Stigand (1915) naye anatoa maelezo machache sana kuhusu lahaja ya Kipemba. Zaidi anaangalia msamiati wa Kipemba unavyofanana au kutofautiana na lahaja nyingine za Kiswahili kama anavyofafanua katika nukuu lifuatalo:

> "…Kipemba ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Inafanana sana na lahaja ya zamani, ina maneno mengi yaliyochukuliwa kutoka wakazi wa zamani wa visiwani" (uk.26).

Hata hivyo, kazi ya Stigand pia haikuonesha tofauti ya msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Naye Ingrams (1924) alilinganisha lahaja mbalimbali za Kiswahili ambazo zinazungumzwa katika visiwa vya Zanzibar. Kazi yake inalinganisha Kiunguja, Kitumbatu, Kimakunduchi na Kipemba. Kuhusu lahaja ya Kipemba anasema:

> "…Wapemba wanazungumza lahaja… inayoitwa Kipemba ambapo inatofautiana tena na Kihadimu na Kitumbatu" (uk 3).

Kazi ya Ingrams zaidi ililinganisha msamiati uliotumika katika lahaja za Kiswahili zinazopatikana Zanzibar yaani Kipemba, Kitumbatu, Kihadimu (Kimakunduchi) na Kiunguja. Kazi yake hiyo haioneshi uchambuzi wa tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini.

Whitely (1958) alichunguza lahaja na mashairi ya Kiswahili yanayopatikana katika kisiwa cha Pemba. Katika utafiti wake aligundua kwamba katika maeneo tofauti ya kisiwa cha Pemba kuna lahaja tofauti zinazozungumzwa. Kwa mfano, eneo la Micheweni - Wingwi (Kaskazini Mashariki ya kisiwa), kisiwa cha Kojani (Mashariki) na Matale (Kusini ya Kojani) na baadae alifanya uchambuzi wa kiisimu. Licha ya juhudi aliyoifanya kazi yake haitoi maelezo ya kina kuonesha uchambuzi wa kiisimu wa tofauti za Kiswahili kizungumzwacho maeneo mbali mbali ya Pemba. Pia hakuonesha tofauti ya msamiati wa lahaja hii kwa Kipemba cha Kaskazini na Kusini.

Polome (1967) alitafiti na kuandika juu ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake. Katika kazi yake anabainisha kuwa Micheweni wanazungumza lahaja ndogo ambayo kwa kiasi fulani inatofautiana na maeneo mengine ya Pemba. Polome (1967:24) anafafanua:

> "Kipemba kinazungumzwa katika kisiwa cha Pemba isipokuwa Pemba Kusini. Ambako hakuna ukakaishaji wa kiambishi **ki-** kabla ya nomino zinazoanza na irabu. katika baadhi ya maeneo kama Micheweni- Wingwi pembe ya Kaskazini lahaja ndogo zimetokea; kwa mfano, Micheweni wanatumia **'ki-'** Badala ya **'h-'** katika kiambishi cha ukanushi wa nafsi ya pili au ya tatu umoja"

Ingawa Polome hakutoa mifano wala hakubainisha tofauti za msamiati wa Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba.

Temu (1980) alitembelea Tanga, Mombasa na sehemu nyingine za pwani ya Kenya kufanya utafiti juu ya lahaja mbali mbali za Kiswahili. Alilinganisha lahaja mbali mbali za Kiswahili zikiwemo lahaja za Zanzibar (Kitumbatu na Kimakunduchi). Katika kazi yake anawakosoa baadhi ya wataalamu walioandika kuhusu lahaja za Kiswahili pale anapoeleza.

> "……inaelekea baadhi ya wataalamu wengine waliviona vilahaja kama lahaja" (uk 12).

Katika utafiti wake licha ya kueleza "lahaja ya Kipemba", Temu kwa mujibu wa maelezo yake yeye mwenyewe, hakufika Pemba. Aidha kazi yake nayo haina uchanganuzi wa tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini.

Batibo (1982) alifanya utafiti kulinganisha lahaja za Kiswahili za Kusini mwa mwambao wa Afrika ya Mashariki. Alitembelea baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara na Unguja mjini. Katika kazi yake anaeleza kuwa lahaja zote zinakaribiana. Batibo anaeleza kuwa:

> "…kufuatana na matokeo haya lahaja zote zinakurubiana kwa vile kwa jumla. Hakuna matatizo katika kuwasiliana baina ya wazungumzaji wa lahaja zote" (uk.6)

Hata hivyo maelezo hayo ya Batibo yanaacha ombo kwa sababu ukiachia watu wazungumzao Kiswahili sanifu, watumiaji wa lahaja nyinginezo wanapata ugumu katika kuwasiliana. Inawezekana Batibo alitafiti maeneo ya mjini tu bila kufika maeneo ya vijijini ambako tofauti za msamiati wa lahaja moja hujitokeza wazi wazi. Khamis (1984), alichunguza tofauti baina ya Kipemba kizungumzwacho mjini na kile cha vijijini. Utafiti wake ulichunguza vipengele mbali mbali vya kiisimu kwa kina lakini bado kuna shaka ambazo hata yeye mwenyewe alizigundua baada ya utafiti wake kukamilika kwamba Kiswahili kizungumzwacho katika maeneo ya vijiji kinatofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka eneo moja hadi jingine. Khamis: (1984:108) analifafanua hili kwa kusema:

> "Tulijikita zaidi (kutafiti) mijini na baadhi ya vijiji vya ndani. Ni wazi kwamba Uchunguzi unahitajika katika vijiji vingine… Uchunguzi huo unahitajika kuanzisha mgao wa lahaja ndogo ulio wazi zaidi. Huu hauelezi kwa kina kulingana na Kutofautiana kwa lahaja ndogo"

Utafiti wa Khamis haukuonesha tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba. Mshindo (1989) alitafiti matumizi ya kiambishi **'ki-'** katika lahaja ya kipemba. Kazi yake ilijikita katika sarufi ya lugha kwa kuchunguza namna kiambishi **'ka'-** kinavyotumika katika mazingira tofauti. Pamoja na juhudi kubwa za mtafiti huyu, kazi yake haielezi tofauti ya msamiati wa Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba.

Maganga (1991) analinganisha lahaja za Kiswahili zinazopatikana katika visiwa vya Zanzibar, Kiswahili sanifu, Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu. Katika utafiti

wake analinganisha mofofonolojia ya lahaja hizi na kubaini kuwa lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba haiko sawa kisiwa kizima, kuna lahaja tofauti kimaeneo hasa katika matumizi. Hata hivyo, kazi yake haikubainisha ni lahaja zipi wala haikuchunguza tofauti za msamiati baina ya lahaja Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba.

Kipacha (2004) aliandika kuhusu lahaja mbali mbali za Kiswahili zipatikanazo katika mwambao wa Afrika ya Mashariki kama vile Chimiini, Kitikuu, Kipate, Kisiu, Kiamu, Chijomvu na Kingare. Lahaja nyengine ni Kivumba, Kimrima, Kipemba, Kiunguja, kimakunduchi, kitumbatu, kimgao na kingome. Katika kazi yake amebainisha tofauti zilizopo baina ya lahaja moja na nyengine akiwa amejikita zaidi katika kipengele cha msamiati na kwa uchache katika vipengele vya fonolojia na miundo. Hata hivyo, kazi ya kipacha haionyeshi tofauti za msamiati wa lahaja ya kipemba cha Kaskazini na Kusini.

Juma (2011) alitafiti tofauti za kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Wete katika kisiwa cha Pemba. Katika utafiti wake aliangalia tofauti za kifonolojia, kimsamiati, kimofolojia. Katika kipengele cha msamiati aliangalia maneno yenye maana sawa au maana zinazokaribiana na yanavyotofautiana kimaumbo na kubainisha tofauti za msamiati kupitia vikoa vya maana.

Tafiti na kazi tangulizi zimemuwezesha mtafiti kugunduwa kuwa kuna ukosefu wa utoshelevu katika ugunduzi wa watafiti katika kueleza lahaja za Kiswahili. Ombo hili la kitaaluma linahitaji kufanyiwa utafiti zaidi ili kuziba pengo lililopo.

2.5 Kiunzi cha Nadharia

Massamba (2004) anaeleza kuwa nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimaelezo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielezo cha kuelezea jambo. Kiunzi cha nadharia ambacho kilitumika katika utafiti huu ni nadharia ya Isimulinganishi**.** Isimulinganishi ni tawi la Isimuhistoria linalojishughulisha na ulinganishaji wa lugha ili kuanzisha uhusiano wake wa kihistoria. Kiunzi hiki cha kinadharia kinachunguza na kuchanganuwa lugha tofauti zenye uhusiano na asili moja. Lehman akinukuliwa na Mgullu (2001:3) anaeleza kuwa lengo mahususi la Isimulinganishi ni kufanya uchunguzi wa lugha mbali mbali ili kuzilinganisha na pia kuzilinganua.

Kupitia kiunzi hiki, wanaisimu huzichunguza lugha katika viwango vyote yaani fonolojia, mofofonolojia, sintaksia na semantiki ili kuonyesha na kuelezea jinsi lugha hizo zinavyofanana au kutofautiana na kutumia mbinu linganishi (Campell, 2004). Kanuni ya msingi ya mbinu hii ni kuzilinganisha lugha mbili au zaidi ili kubainisha tofauti na mabadiliko ya mifumo ya fonolojia, mofolojiana sintaksia inavyojitokeza. Mnamo mwaka 1972 nadharia hii ilitumiwa na Raimo Antilla kulinganisha lugha za Kiswidi, Kiingereza na Kijerumani. Antilla (1972:229) anaeleza:

> "…ni mbinu kuu ya isimu linganishi inayotumiwa kuchambua lugha zaidi ya moja ambazo zina asili moja ili kuanzisha uhusiano wake wa kihistoria."

Katika nadharia ya isimu linganishi kuna vigezo vitatu vinavyotumiwa kulinganisha lugha. Kigezo cha kwanza ni msamiati wa msingi. Huu ni msamiati unaohusu vitu vya kawaida katika mazingira ya wasemaji wa lugha zinazohusika, vitu vilivyo vya asili katika mazingira hayo, majina ya viungo vya mwili na shughuli za kila siku za

jamii inayohusika. Kigezo cha pili ni kukubaliana kwa sauti katika maneno, kulinganisha sauti za msamiati wa msingi ili kuona ni kwa kiasi gani zinafanana au zinatofautiana. Kigezo cha tatu ni kuchunguza ili kuona kama lugha hizo zina maneno yenye maana moja lakini yana sauti tofauti. Maneno yanatofautiana kimaumbo lakini yakiwa na ukubalifu wa sauti hujujikana kama maneno mnasaba (Massamba,2002:40-43). Nadharia hii ilitumika katika utafiti huu katika kutofautisha msamiati wa lahaja ya kipemba cha Kaskazini na Kusini.

Aidha, katika karne ya 20 mwanaisimu Morris Swadesh alianzisha mbinu ya takwimu leksika (Swadesh list). Mbinu hii ya Swadesh hutumia orodha fupi za maneno mia kulinganisha msamiati wa lugha zinazochunguzwa. Hata hivyo, mbinu linganishi baadhi ya wakati huonekana kuwa na kasoro kwani huishia kuonyesha uhusiano wa vipengele vya lugha hizo tu (Campell, 2004). Ili kuzuia kasoro hiyo, mbinu ya uchambuzi wa matini (mazungumzo) za lugha asilia ilizingatiwa katika utafiti huu.

2.6 Muhutasari

Sura hii inabainisha na kuelezea mapitio ya kazi tangulizi. Katika kueleza mapitio ambayo yametumika katika utafiti huu tumeelezea tafiti za lahaja ulaya na Marekani, Afrika na Utafiti wa lahaja za Kiswahili. Pia sura hii inaelezea kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu na mwisho ni muhutasari wa sura.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mbinu za utafiti ambazo mtafiti alizitumia katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele vinavyobainishwa katika sura hii ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na mbinu za ukusanyaji wa data. Pia sura hii inaelezea mbinu za uchambuzi wa data uwasilishaji, maadili ya utafiti na muhutasari wa sura hii.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Kisiwa cha Pemba, kisiwa dada na Unguja katika visiwa vya Zanzibar. Kisiwa cha Pemba kiko katika bahari ya Hindi umbali wa kilomita 40 katika Mwambao wa Afrika Mashariki. Kisiwa hiki kina ukubwa wa kilomita za mraba 984. Kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 kisiwa hiki kilihesabiwa kuwa na wakazi wapatao 406,455 ambao hujulikana kama Wapemba. Kiutawala, kisiwa hiki kimegawika mikoa miwili ambayo ni mkoa wa Kaskazini na mkoa wa Kusini.

Kwa mujibu wa Juma (2011:1) lugha mama ya Wapemba ni Kiswahili kinachojulikana kama ‘lahaja ya Kipemba’. Wazungumzaji wa lahaja hii hutofautiana kilafudhi, kimsamiati usio wa msingi, kimaumbo na hata baadhi ya miundo ya sentensi kutoka eneo moja na jingine. Kwa mfano, Kipemba kinachozungumzwa Micheweni ni tofauti na kile kinachozunguzwa Kojani, hali

kadhalika Kipemba kizungumzwacho Vitongoji ni tofauti na kile cha Mwambe, Kangani na Chokocho. Katika kuchunguza tofauti za kimsamiti utafiti huu ulifanyika katika vijiji vya Micheweni, Kiuyu Mbuyuni na Maziwang'ombe ambavyo vinapatikana katika wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini. Kwa upande wa Mkoa wa Kusini tulichunguza msamiati katika maeneo ya vijiji vya Mwambe, Kangani na Chokocho ambavyo vipo wilaya ya Mkoani. Sababu za uteuzi wa maeneo hayo ni uzoefu alionao mtafiti na wepesi wa mtafiti kuweza kupata uenyeji na kuhudumiwa, kutumia muda wake wa ziada katika kukusanya data.

3.3 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo kwa mujibu wa Cohen na wenzake (2000) ni kupanga kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Data zinapangwa kutokana na maudhui au makundi yanayolingana. Muundo huu ni muhimu kwani ulimsaidia mtafiti kufafanua dhana zilizofungwa, na pia maelezo yaliyotolewa na washiriki yalitolewa ufafanuzi wa kina. Utafiti huu ulitumia njia ya dodoso, mahojiano na ushuhudiaji katika kukusanya data. Data zilizotumika ni za kimaelezo ambazo zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa.

3.4 Walengwa wa Utafiti (Usampulishaji)

Cooper (1989) na Vans (1990) wanafasili kundi lengwa kuwa ni wanachama wote au hata, mtu mmoja, kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kwa mujibu wa Adamu (2008) usampulishaji ni mbinu, mchakato au

kitendo cha kuwatafuta walengwa wa utafiti. Kwa hiyo walengwa wa utafiti huu walikuwa ni wakazi wote wa Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba.

3.5 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli ni istilahi inayotumika kumaanisha watu walioteuliwa kujibu maswali ya utafiti kutoka katika kundi husika (Kothari, 1990) ambapo Cohen na wenzake (2010) wanaeleza kuwa sampuli ni kiwakilishi cha watafitiwa waliokusudia kutoa taarifa za utafiti.

Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwahoji watu wote wanaoishi katika kisiwa cha Pemba, mtafiti alifanya uteuzi wa sampuli ili kupata kundi dogo la watu waliofanyiwa utafiti ambalo liliwakilisha kundi kubwa. Mtafiti alichagua maeneo maalumu kufanyia utafiti wake ambapo ni wilaya ya Micheweni kwa mkoa wa Kaskazini na Wilaya ya Mkoani kwa Mkoa wa Kusini.

Utafiti huu ulitumia sampuli tegemea-fursa (probability sampling) ambayo ilimsaidia mtafiti kupata watafitiwa wale anaowataka tu kwa uwakilishi sawa wa kila kundi. Sampuli tegemea-fursa na sampuli eneo (area sampling) zilitumika kwa sababu tulichagua watafitiwa kwa vigezo vya umri, elimu na ukazi. Kila kijiji teule walihojiwa watu kumi . Pia walimu thelathni (30) walipewa madodoso na kuyajaza ambapo walimu 5 waliteuliwa kutoka katika shule ziliopo katika vijiji vilivyoteuliwa na mtafiti kuwa ndio maeneo ya utafiti.Katika utafiti huu sampli tegemea fursa na sampuli eneo zilitumika katika kukusanya data alizo zihitaji mtafiti ili kujibu maswala ya utafiti wake kwa wale tu aliowateuwa ambapo ni wakaazi wa vijiji vilivyoteuliwa kwa kutumia snow ball style(sampuli tajwa) ambapo watafitiwa walitajana ili mtafiti kupata data anazozihitaji.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti huu mbinu mbalimbali zilitumika katika kukusanya data. Kothari (1990) anaifafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikia kwenye malengo yake ya utafiti. Aidha anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu tatu za ukusanyaji wa data ambazo ni Dodoso, Mahojiano na Ushuhudiaji.

3.6.1 Mbinu ya Dodoso

Kwa mujibuwa Kothari (1990) dodoso ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandalia maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemea taarifa inayohitajika na mtu anaepewa dodoso hizo.

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kukusanya data ambazo anaamini alizipata kutoka kwa wamilisi wa lugha katika maeneo husika. Katika utafiti huu mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini katika vijiji teule. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliwapa dodoso walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule zilizomo katika vijiji tafitiwa, jumla ya walimu 30 walipewa maswali ya dodoso. Katika kila shule walimu watano walipewa madodoso na kuyajaza. Mbinu hii imeweza kujibu swali la kwanza la utafiti huu. Katika mbinu hii mtafiti alipata majibu ambayo hayaelewi vizuri, hivyo

mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano ili kupata ufafanuzi wa mapungufu yaliyojitokeza katika mbinu hii.

3.6.2 Mbinu ya Mahojiano

Mbinu hii humruhusu mtafiti kukunsanya data akiwa ana kwa ana na mtafitiwa, huuliza maswali na kurikodi katika daftari la kumbukumbu au kinasa sauti. Kwa mujibu wa Kothari (1990) mahojiano ni mbinu ya kukusanya data inayohusu mchakato wa kuuliza maswali ambapo mtafiti anaweza kufafanua maswali ambayo hayaeleweki na mtafitiwa. Uteuzi wa mbinu hii ni kwa sababu ilisaidia kupata watafitiwa wanaojua kusoma na kuandika na wasiojua kusoma, taarifa za uhakika ziliweza kupatikana kwa vile mtafiti alikuwa na mlahaka mzuri na mashirikiano na watafitiwa. Hii ni mbinu iliyotumika kwa kiwango kikubwa zaidi kwani ndiyo iliyompa mtafiti taarifa za awali na uhakika kwa alichokitafuta. Ingawa inapoteza muda kwa vile kumfuata mtafitiwa mahali alipo lakini ilisaidia kupata vielelezo vya uhakika. Mbinu hii iliweza kujibu swali la pili la utafiti huu ambalo ni kupata sababu zilizopelekea utofauti wa kimsamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini.Kundi lengwa lililohusishwa na mbinu hii ni watu wenye umri wa miaka 50-75 na 25-49. Katika mbinu hii iliwezekana baadhi ya watafitiwa kuona aibu au uoga na kusababisha kutoa taarifa ambazo si za uhakika ili kuondoa mapungufu hayo mtafiti alitumia mbinu za ushuhudiaji.

3.6.3 Mbinu ya Ushuhudiaji

Katika mbinu hii, mtafiti hukusanya taarifa kwa kushuhudia au kushiriki katika mazingira halisi. Mtafiti aliweka kumbukumbu za taarifa ambazo anazihitaji katika

daftari na sehemu maalumu aliyoiweka makusudi kwa kazi hii. Adam (2008) anasema kuwa matumizi ya mbinu hii ni lazima mtafiti awepo kwenye uwanda na ili kupata taarifa kwa usahihi ni lazima atumie viungo vya hisia ikiwemo kuona, kusikia, kugusa, kunusa na kuonja. Ili ushuhudiaji uwe wenye kuleta mafanikio, mtafiti atakuwa makini katika kuandika taarifa, kuvifikia vipengele vyote anavyotaka kuvishuhudia na kuwa na muda wa kutosha. Manufaa ya mbinu hii ni kuwa mtafiti alipata ufahamu wa kutosha kuhusu mada anayoitafiti, pia kuielewa vyema jamii anayoifanyia utafiti.

Pamoja na hayo mbinu hii iliweza kuwa na mapungufu kwa vile watafitiwa waliojuwa kuwa wanafuatiliwa waliweza kufanya mambo tofauti na uhalisia wake.

Katika utafiti huu mbinu hii ilitumika kwa kumpa fursa mtafiti kuweza kushiriki katika shughuli mbali mbali za kijamii ambapo atapata kusikia msamiati unaotumika katika vijiji hivyo. Mbinu hii ilijumuisha na mbinu ya masimulizi ili kumsaidia mtafiti kupata taarifa za utafiti zaidi. Katika utafiti huu mbinu hii ilijibu suali la kwanza na la pili ikiwa ni kubaini msamiati na kuelewa sababu za utofauti wa msamiati huo wa lahaja za Kipemba cha Kaskazini na Kusini Pemba.

3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa katika utafiti huu, zilichambuliwa kwa njia ya maelezo na majedwali kwa uchambuzi wa kihesabu. Data ambazo zilichambuliwa kwa njia ya majedwali pia zilifafanuliwa zaidi kwa kuwekewa maelezo. Pia, mtafiti alitumia mbinu ya uhakiki wa maelezo katika uchambuzi wa data wakati wa kuchambua mazungumzo na masimulizi. Kipengele cha kileksika katika sarufi kilitumika katika kupambanua tofauti za msamiati zilizojitokeza katika utafiti huu.

3.8 Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa katika tasinifu ambayo imegawanywa katika sura tano ambapo kila sura imechukua kipengele mahususi. Sura ya kwanza ni utangulizi, sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi, sura ya tatu ni mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data, sura ya nne ni matokeo ya utafiti na sura ya tano ni muhutasari, mapendekezo na hitimisho. Katika upangiliaji wa sura, kila sura inaanza na utangulizi, ikifuatiwa na maelezo ya mjadala na kuishia na muhutasari.

3.9 Maadili ya Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti alieleza maadili kwa watafitiwa ili kutoa taarifa za kweli bila ya woga. Kwa mujibu wa Sture (2010) mkabala wa maadili ni mojawapo ya maswala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Pia Adam na wezake (2008) wametaja maadili ya utafiti ni haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hatatoa siri za mtafitiwa. Anafafanua kuwa haki ya mtafitiwa ni kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalo penda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alitambua haki zote hizi na kuzifanyia kazi ambapo aliwaeleza watafitiwa kuwa pindipo kutatokea tatizo ni jukumu la mtafiti.

3.10 Muhutasari

Katika sura hii tumeeleza mbinu za utafiti ambazo mtafiti alizitumia katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele ambavyo vimebainishwa ni muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na mbinu za ukusanyaji wa data. Pia tumeelezea mbinu za uchambuzi wa data uwasilishaji, maadili ya utafiti na muhutasari wa sura hii.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inajadili tofauti za kimsamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Wakati tunajadili tofauti hizo tuliangalia namna maneno yenye maana sawa au maana zinazokaribiana yanavyotofautiana kimaumbo. Tofauti hizo za maneno tumezigawa katika makundi matatu; yaani, tofauti za kimatamshi, tofauti za kimofolojia na tofauti za kimaumbo. Mwisho, sura inabainisha sababu za tofauti za msamiati. Lakini kabla kubainisha tofauti hizo sura hii imeanza kueleza machache kuhusu msamiati wa lahaja ya Kipemba.

4.2 Msamiati wa Kipemba

TUKI (2004:272) wanafasili msamiati kuwa ni *jumla ya maneno katika lugha*. Kuna wataalamu ambao wamewahi kutafiti na kuandika kazi mbalimbali kuhusu msamiati wa lahaja ya Kipemba. Miongoni mwa wataalamu hao ni Ingrams (1924), Whiteley (1958), Polome (1967), Nurse (1982), Khamis (1984), Maganga (1991) na Kipacha (2004).

Lakini kabla hatujajielekeza katika lengo la sehemu yetu ya kwanza, litakuwa jambo la busara sana angalau tukaelezea machache kuhusu wataalamu walioandika msamiati wa Kipemba. Kwani hadi hivi sasa bado hakuna maelezo ya kutosha katika

kazi nyingi zinazobainisha msamiati wa Kipemba. Hali hiyo ya mambo kutokuwa bayana inatokana na mambo yafuatayo:

4.2.1 Kutofanywa Utafiti wa Kina

Kama tulivyodekeza katika sura ya kwanza ya tasinifu hii, mpaka sasa hakuna utafiti wa kina uliofanywa kulinganisha msamiati wa lahaja ya Kipemba katika maeneo mbalimbali. Kwa mujibu wa tajiriba na uelewa wa mtafiti, tafiti zilizofanywa angalau kwa umakini kidogo na kwa kina kuhusu msamiati wa "lahaja ndogo" za Pemba ni ule wa Khamis (1984) na Juma (2011). Kwa sababu hiyo, baadhi ya kazi tangulizi zilizoandikwa na wataalamu hao zina kasoro kadhaa katika kubainisha msamiati wa lahaja ya Kipemba. Baadhi ya kazi hizo zinabainisha kuwa lahaja ya Kipemba hutofautiana kimsamiati baina ya eneo moja na jingine lakini hakuna maelezo ya kutosha kuhusu hali hiyo.

4.2.2 Kipemba Kutokuwa na Msamiati Mmoja

Kuna baadhi ya wataalamu walioandika msamiati wa lahaja ya Kipemba huchukulia kuwa lahaja hii inazungumzwa sawa kisiwa kizima. Hivyo basi, wataalamu hao huilinganisha na lahaja za maeneo mengine kama vile Kitumbatu, Kiunguja, Kimtang'ata, Kimrima na/au Kisanifu. Jambo hili sio sahihi kwa sababu lahaja ya Kipemba inatofautiana kwa baadhi ya vipengele vya kiisimu ukiwemo msamiati baina ya eneo moja na jingine. Tofauti hizo zimethibitishwa na Whitely (1958) zikashadidiwa na Khamis (1984) na kuzidi kuwekewa mwega na Juma (2011).

4.2.3 Ukosefu wa Vyanzo vya Data

Kasoro nyingine inayozikabili kazi tangulizi zilizoandikwa kuhusu lahaja ya Kipemba ni ukosefu wa vyanzo vya data. Kazi nyingi zilizochunguza msamiati wa lahaja ya Kipemba, tukiacha ile ya Khamis (1984) na ya Juma (2011) hazibainishi vyanzo halisi vilivyotumika wakati wa ukusanyaji wa data. Kwa mfano, kazi hizo hazitaji watoa taarifa na mahali pa utafiti. Jambo hili limefanya kazi nyingi kuwa na makosa, kwa mfano msamiati wa eneo fulani unaweza ukajumuishwa kuwa ni msamiati wa Pemba yote na pengine ni kinyume chake.

4.2.4 Ukosefu wa Maelezo ya Kina

Ukosefu wa maelezo ya kina ni kasoro nyingine inayozikabili kazi tangulizi kuhusu msamiati wa lahaja ya Kipemba. Hadi sasa hakuna kazi yenye maelezo ya kutosha inayofafanua vyanzo vya msamiati wa Kipemba katika maeneo mbalimbali ya kisiwa hiki. Hivyo basi, kazi hizo hazibainishi upi ni msamiati wa asili wa Kipemba na upi ni msamiati uliokopwa kutoka lugha za kigeni kama vile Kiarabu, Kiingereza na Kireno. Mambo hayo tuliyoyabainisha yanahitaji kuzingatiwa na wanaisimu kwa sababu huleta kasoro za kitaaluma pale ambapo pametokea msigano baina ya wataalamu wawili wanaozungumzia kitu kimoja. Tulishadokeza hapo awali kuwa katika sehemu hii tutabainisha na kujadili tofauti za kimsamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Tofauti za kimsamiati za lahaja za maeneo hayo zinajidhihirisha katika hali tatu: ambazo ni tofauti za kimatamshi, tofauti za kimofolojia na tofauti za kimaumbo ya maneno.

4.3 Tofauti za Kimatamshi

Katika sehemu hii tunakusudia kubainisha lengo mahususi la kwanza la utafiti huu. Lengo letu linataka kubainisha tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Kwa mujibu wa data yetu ilopatika kutokana na mbinu ya dodoso,Mahojiano na ushuhudiaji zimedhihirika kuwa kuna tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini zitokanazo na tofauti za kimatamshi. Kihore na wenzake, (2001:19) wanafasili *matamshi* kuwa ni utaratibu maalumu wa utoaji wa sauti za lugha kwa kutumia chemba ya kinywa na chemba ya pua. Utaratibu huo maalumu wa utoaji wa sauti huhusu *namna* au *jinsi* ya kuzitoa sauti hizo na *mahali* ambapo sauti hizo hudhibitiwa. Kwa hiyo, kuna baadhi ya maneno ambayo wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini hutofautiana na wale wa Kusini katika utamkaji ambapo sauti fulani ya neno hubadilishwa na kutamkwa sauti nyingine. Tofauti hizo huyafanya maneno yaonekane tofauti kifonetiki japokuwa yana maana sawa au zinazokaribiana.

4.3.1 Tofauti za Mpishano wa Sauti

Kama tulivyodokeza hapo juu kuna tofauti za kimsamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinazotokana na mpishano wa sauti. Tofauti hizo zinajibainisha katika mpishano wa konsonanti, mpishano wa irabu, mpishano wa nusu-irabu na udondoshaji wa sauti, ukakaishaji, lafudhi, mpumuo na kibenua ulimi. Tofauti hizo huyafanya maneno yenye maana sawa au maana zinazokaribiana zitofautiane sehemu fulani ya sauti.

4.3.2 Mpishano wa Konsonanti

Kuna baadhi ya maneno ambayo wasemaji wa Kipemba cha Kaskazini hutofautiana na wale Kusini katika utamkaji ambapo sauti fulani ya neno hubadilishwa na kutamkwa sauti nyingine. Mpishano huu wa sauti ni mpishano huru kwa sababu haubadilishi maana ya maneno. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.1: Mpishano wa Konsonanti

Kaskazini	Kusini	Tofauti	Tafsiri
tunturi	sunsuri	t:s	‘sunsuri’
birika	bilika	r:l	‘birika’
bupuru	bufuru	p:f	‘bupuru’
guwa	Buwa	g:b	‘buwa’
kyano	chano	ky:ch	‘chano’
vumbi	dumbi	v:d	‘vumbi’
joma	goma	j:g	‘joma’
repuleni	Zepuleni	r:z	‘ndege’
zeme	veme	z:v	‘zeme’
dapia	Dakia	p:k	‘chupia’
vuga	buga	v:b	‘sumbua’
dukuwa	bukuya	d:b/w:y	‘kata’
chachata	Chachaga	t:g	‘fua’
kesa	chesa	k:ch	‘kesa’
shushuka	Chuchuka	sh:ch	‘kua’
shonya	bonya	sh:b	‘sonya’
kovyoka	Govyoka	k:g	‘tapika’

Mifano katika jedwali (na. 1) hapo juu tunaona kuwa kuna tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinazotokana na mpishano wa konsonanti. Kwa mfano, tofauti hizo zimejibainisha katika mpishano wa konsonanti t:s, r:l, p:f, g:b, ky:ch, v:d, j:g, na kadhalika.

4.3.3 Mpishano wa Irabu

Pia, tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinajibainisha katika mpishano wa irabu. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.2: Mpishano wa Irabu

Kaskazini	Kusini	Tofauti	Tafsiri
boje	Buje	o:u	‘uvimbe’
vukuto	vukuti	o:i	‘vukuto’
izia	Uzia	i:u	‘uzia’
egema	igama	e:i/a	‘egemea’
puma	poma	u:o	‘pumua’

Katika mifano hiyo tunaona kuwa kuna tofauti za utamkaji wa msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Tofauti hizo zinatokana na mpishano wa irabu katika nomino. Kwa mfano, tumebaini mpishano wa o:u, o:i, i:u na kadhalika.

4.3.4 Mpishano wa Nusu Irabu

Aidha, tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zinaonekana katika mpishano wa nusu-irabu au viyeyusho. Tuangalie mifano ifuatayo katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4.3: Mpishano wa Nusu-Irabu

Kaskazini	Kusini	Tofauti	Tafsiri
bauwu	bauyu	w:y	‘mkojo’
pwaa	Pyaa	w:y	‘bahari’
tambuwa	Tambuya	w:y	‘tambua’
juwa	Juya	w:y	‘jua’
vuwa	vuya	w:y	‘vua’

Katika mifano hiyo tunaona kuwa kuna tofauti za utamkaji wa nomino baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini kutokana na mpishano wa nusu-irabu. Kwa mfano, watu wa Kaskazini wanapo weka ‘w’ kusini huweka ‘y’.

4.3.5 Udondoshaji wa Sauti

Vilevile, kuna tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zitokanazo na udondoshaji wa sauti. Katika sauti hizo watu wa Kaskazini hudondosha sauti fulani lakini watu wa Kusini huichopeka sauti hiyo. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.4: Udondoshaji wa Sauti

Kaskazini	Kusini	Tofauti	Tafsiri
bankuu	Bankuyu	-:y	‘kaka wa baba’
chepeu	Chepeyu	-:y	‘chepeu’
jiwe	Jibwe	-:b	‘jiwe’
dagaa	dagaya	-:y	‘dagaa’
funguo	Funguyo	-:y	‘funguo’
funza	Fuza	n:-	‘funza’

ungo	yungo	-:y	‘ungo’
ugwe	yugwe	-:y	‘kamba’
eleka	Kweleka	-:kw	‘beba’
bwakia	Akia	bw:-	‘akia’
oza	Yoza	-:y	‘ozesha’
okota	yokota	-:y	‘okota’
inga	Winga	-:w	‘inga’

Katika mifano hiyo tunaona kuwa kuna tofauti za utamkaji wa maneno baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zitokanazo na udondoshaji wa sauti kwa baadhi ya maneno. Kupitia mifano tunaona watu wa Kaskazini wanadondosha baadhi ya sauti na watu wa kusini wanapachika sauti.

4.3.6 Tofauti za Ukakaishaji wa Sauti

Massamba (2004:99) anafasili *ukakaishaji* kuwa ni utamkaji wa sauti ambao kwao sehemu ya mbele ya ulimi husukumwa nyuma kuelekea kwenye kaakaa. Ukakaishaji hufanya sauti isiyo ya kaakaa gumu kutamkwa katika uelekeo wa kaakaa gumu. Kwa hiyo, kuna tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini tunaziona katika ukakaishaji. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo hapa chini:

Jedwali Na. 4.5: Ukakaishaji wa Sauti

Kaskazini	Kusini	Tafsiri
kyama	*chama*	‘chama’
Kyoo	*Choo*	‘choo’
Kyungu	*Chungu*	‘chungu’
Kyeupe	*cheupe*	‘cheupe’

Katika mifano hiyo, sauti [ch] ambayo ni kizuio kwamizi kisoghuna cha kaakaa gumu hutamkwa kama ilivyo katika Kiswahili sanifu kwa upande wa Kusini lakini sauti hiyo hutamkwa [ky] ambayo ni kizuio kwamizi kisoghuna cha kaakaa laini kwa upande wa Kaskazini.

Polome (1967:24) anadokeza kwamba ukaakaishaji unaonyesha uasili zaidi unapotokea kabla ya [i] pekee kwa sababu [i] ni irabu ya mbele zaidi kuliko [e]. Kwa mfano *ki+angu > kyangu changu.* Katika hali hiyo tunaona kuwa [k] inabadilika kuwa [ch] katika mazingira fulani. Kwa hivyo, msamiati wa Kipemba cha Kaskazini ni wa kilahaja zaidi ukilinganishwa na ule wa Kipemba cha Kusini.

4.3.7 Tofauti za Lafudhi

Massamba na wenzake (2004:10) wanaeleza kuwa lafudhi ni sifa ya kimasikizi ya matamshi ya mtu binafsi ambayo humpa msemaji utambulisho fulani ama kijamii au kieneo. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba lafudhi hutokana na athari za mazingira ya mtu kijamii au kijiografia. Lafudhi huweza kumtambulisha mtu kijiografia kwa sababu baadhi ya wazungumzaji huathiriwa sana na mazingira yao ya kijiografia au lugha zao za mwanzo.

Kwa hivyo, kuna tofauti za kimsamiati zitokanazo na tofauti ya lafudhi baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Kwani watu wa Kaskazini katika maeneo kama vile Micheweni, Kiuyu na Maziwang’ombe lafudhi yao hubainika waziwazi na huwafanya waweze kujulika kutokana na utamkaji wao wa maneno.Tofauti hizi zilipatikana kwa mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji ambapo mtafiti alipata kusikia

jinsi gani maneno yanatamkwa na kuweza kubaini tofauti ya lafudhi. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.6: Tofauti za Lafudhi

Kaskazini	Kusini	Tafsiri
mwambile	*mwambie*	‘mwambie’
hikile	*Kile*	‘kile’
Shungwa	*chungwa*	‘chungwa’
kyakwe	*chake*	‘chake’

Katika mifano hiyo, tunaona kuwa katika Kipemba cha Kaskazini maneno hutamkwa tofauti na Kipemba cha Kusini. Tofauti hizo za kimatamshi na kimasikizi huwafanya watu wa Kaskazini na Kusini waweze kutambulikana wanapozungumza na watu wa maeneo mengine ya kisiwa cha Pemba.

4.3.8 Tofauti za Matumizi ya Mpumuo

TUKI (1990:7) wanafasili *mpumuo* kuwa ni pumzi kali inayojitokeza wakati wa utamkaji wa baadhi ya vitamkwa. Katika Kiswahili sanifu mpumuo hauonyeshwi kama ni sifa muhimu katika lugha hii. Lakini hadi hii leo mpumuo umeshamiri na hujitokeza waziwazi katika utamkaji wa vitamkwa **p, k, t** na **ch.** Mpumuo hutumiwa na wasemaji wazawa wa Kiswahili wa pwani na wasemaji wa lahaja nyinginezo za Kiswahili. Matumizi ya mpumuo ni tofauti nyingine ya utamkaji wa msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini.Mtafiti alipata data ya matumizi ya mpumuo kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji na mahojiano ambapo mtafiti alipata kusikia maneno jinsi yanavyotamkwa na kuweza kugungua kuwa kuna matumizi ya

mpumuo katika maneno ya lahaja ya Kipemba. Tuangalie mifano katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4.7: Matumizi ya Mpumuo

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
kamba	*k^{h}amba*	‘kamba’
Kata	*k^{h}ata*	‘kata’
kat^{h}a	*k^{h}ata*	‘kata’
utomvu	*ut^{h}omvu*	‘utomvu’
kit^{h}u	*k^{h}it^{h}u*	‘kitu’

Katika mifano hiyo, tunaona kuwa kuna tofauti za matumizi ya mpumuo baina Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Licha ya matumizi tofauti ya mpumuo, maneno tuliyoyabainisha katika mifano hapo juu yana maana sawa baina ya Kaskazini na Kusini.

4.3.9 Utokeaji wa Kibinuaulimi [nd^r]

Kibinuaulimi ni kitamkwa ambacho hutolewa wakati ulimi ukiwa umesukumwa mbele lakini ncha ya ulimi ikiwa imeelekezwa kwenye kaakaa gumu (Massamba, 2004:30). Katika Kipemba cha kaskazini kuna utokeaji wa sauti ya kibinuaulimi [nd^r] wakati katika Kipemba cha Kusini hakuna utokeaji wa sauti hiyo.Mtafiti aligungua matumizi ya kibenua ulimi kutokana na mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji aliyoitumia katika kukusanya data kwani ilimpa fursa ya kusikia jinsi maneno yanayotamkwa kutoka kwa watafiti. Tuangalie mifano ifuatayo katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4.8:Utokeaji wa kibinuaulimi [nd^r]

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
nnd^refu	*nrefu*	‘mrefu’
$annd^r$i	*anri*	‘amri’
nnd^rama	*nrama*	‘mrama’
nnd^risho	*nrisho*	‘mrisho’
nnd^rau	*nrau*	‘mrau’

Mifano hiyo inatuonyesha utokeaji wa sauti ya kibinuaulimi [nd^r] katika Kipemba cha Kaskazini. Sauti hiyo hutokea pale sauti [m], ambayo ni nazali ya midomo inapokaribiana na sauti [r], ambayo ni kimadende cha ufizi. Ni vema tuelewe kwamba katika lahaja ya Kipemba sauti [m] inapotokea kusimama peke yake kama silabi hubadilika na kuwa [n]. kwa sababu katika hali halisi nazali ya midomo [m] hubadilika kuwa nazali ya ufizi [n] katika maneno yote ikiwa itafuatiwa na konsonanti isipokuwa konsonanti [p, b, f na v] . Hivyo, sauti [m] inapokutana sauti [r] hufanyika mchakato ufuatao m+r > n+r > nd^r (m>n>n+r > nd^r). katika mchakato huu ndio panapotokea kibenua ulimi katika Kipemba cha Kaskazini.

4.4 Tofauti za Kileksika (Maumbo)

Kwa upande wa tofauti za maumbo ya maneno kuna baadhi ya maneno au matumizi ya maneno ambayo hujitokeza katika Kipemba cha Kaskazini lakini hayatumiki katika Kipemba cha Kusini. Japokuwa maumbo ya maneno hayo yanatofautiana lakini yana maana sawa au iliyokaribiana kisemantiki. Tofauti hizi za maumbo ya maneno ndio huitwa tofauti za kileksika.

4.4.1 Tofauti za Leksika

Hali kadhalika kuna tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Tofauti hizi hutokana na maumbo ya maneno (leksika). Tuangalie mifano ifuatayo katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4.9: Tofauti za Kileksika

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
Kidudu	mdeke	‘uume wa mtoto’
Nchamo	bacha	‘mkeka mkongwe’
Lepe	bangwe	‘kuhisi usingizi’
Kibunju	bera	‘mtoto wa kiume’
gunda	dundu	‘baragumu’
Tumbwija	bavi	‘lengelenge’
komo	bingu	‘komo’
totovu	bunju	‘bunju’
Tumbwi	daka	‘dafu changa’
Geleka	aga	‘potea’
Tilifu	angamia	‘angamia’
Asiza	asa	‘zuia mtoto kunyonya’
Fikicha	bigija	‘finya’
Vova	boba	‘haribika’
Zidiwa	chachiwa	‘zidiwa’
Cheleya	shuka	‘shuka’
Himiza	faulisha	‘himiza’

Katika mifano hiyo tunaona kuwa kuna tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Tunabaini kuwa maumbo ya maneno hayo yanatofautiana lakini yana maana sawa au iliyokaribiana kisemantiki.

4.4.2 Tofauti za Kimofolojia kwa Baadhi ya Maneno

Kuna tofauti za kimsamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini zitokanazo na tofauti za kimofolojia. Katika sehemu hii tutaangalia namna baadhi ya maneno ya

Kaskazini yanavyotofautiana kimofolojia na maneno ya Kusini yenye maana sawa au zinazokaribiana. Tofauti hizo zinapatikana katika udondoshaji wa sehemu ya neno.

Kuna tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini zitokanazo na udondoshaji wa sehemu ya neno. Tuangalie mifano ifuatayo katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4.10: Tofauti za Kimofolojia

Kaskazini	**Kusini**	**Tofauti**	**Tafsiri**
kamange	*kayamange*	-:ya	‘kamange’
gurubi	*gubi*	ru:-	‘gubi’
wayo	*wayowayo*	-:wayo	‘wayo’
Sheli	*shelisheli*	-:sheli	‘shelisheli’
Boko	*bokoboko*	-:boko	‘bokoboko’
Yungi	*yungiyungi*	-:yungi	‘yungiyungi’

Katika mifano hiyo tunabaini kuwa kuna tofauti za maumbo ya maneno ya Kipemba cha Kaskazini hayatumiki katika Kipemba cha Kusini. Kwa mfano, katika Kipemba cha Kaskani hutamka kamange kwa kudondosha ‘ya’ ambapo katika Kipemba cha Kusini huweka ‘ya’ na kutamka kayamange. Licha ya kutofautiana maumbo, maneno hayo yana maana sawa.

4.5 Sababu za Tofauti za Msamiati

Katika sehemu hii tunajaribu kubainisha lengo letu mahususi la pili ambalo ni kueleza sababu zinazopelekea tofauti za kimsamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Tumeweza kuona sababu kadhaa zilizobainishwa na watoa taarifa kuwa

zinapelekea tofauti za Kimsamiati baini ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Miongoni mwa sababu hizo ni kama zifuatavyo hapa chini.

4.5.1 Umbali wa Maeneo Kijiografia

Sababu mojawapo ni watu wanapohamia kwenye maeneo mapya hutengwa na makundi mengine ya wazungumzaji wa lugha hiyo kwa mipaka ya kijiografia, kama vile mito, misitu, na milima. Baada ya kukaa hivyo kwa muda mrefu lugha ya watu hao huanza kutofautiana kwa kiasi fulani kimatamshi, kimsamiati na kimaana na ile ya asili japo kuwa inakuwa imefanana nayo kwa kiasi kikubwa.

Massamba (2004) anaunga mkono hoja hii pale anapoeleza kwamba wasemaji wa lugha moja wanaweza kutofautiana kiusemaji kulingana na maeneo walikosambaa. Kwani huu ndio msingi wa lahaja ambapo huakisi tofauti za lugha zinazojitokeza miongoni mwa wazungumzaji wa lugha moja wanapoachana kijiografia. Wazungumzaji hao wanaweza kutofautiana kimatamshi na pia katika baadhi ya msamiati na hata kimaana ambapo katika lugha ya Kiswahili tofauti hizo zinadhihirika katika lahaja zake.

Kwa hivyo, katika utafiti huu tumebaini tofauti za kimsamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini zitokanazo na mwachano wa maeneo ya kijiografia. Sababu hii inabainishwa na data ya utafiti inayoonesha tofauti za kimatamshi. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.5.1: Sababu za Mwachano wa Kijiografia

Kaskazini	Kusini	Tofauti	Tafsiri

kyano	*chano*	ky: ch	‘chano’
dapia	*dakia*	p:k	‘chupia’
dukuwa	*bukuya*	d:b	‘kata’
kesa	*chesa*	k:ch	‘kesa’
kovyoka	*govyoka*	k:g	‘tapika’

Mifano katika jedwali hapo juu inatubainishia tofauti za msamiati zitokanazo na sababu ya umbali wa maeneo kijiografia. Kutokana na mwachano wa kijiografia kati ya watu wa Kaskazini na Kusini kumeweza kupelekea tofauti za kimatamshi kwa baadhi ya msamiati wa lahaja hizi.

Kwa mujibu wa data yetu sababu hii inaoneshwa kwa jumla ya maneno 53 kati ya ma neno 143 sawa na asilimia 37% yanaonesha sababu ya tofauti ya msamiati inayotokana na muachano wa kijiografia.

4.5.2 Sababu za Kihistoria

Kimsingi inadaiwa kwamba lahaja za Kiswahili ni lugha zenye chimbuko moja ambazo zimepata kuachana na kugawanyika na kuwa lahaja (Massamba, 2007). Kutokana na sababu za kihstoria lahaja za kiswahili zinatokana na lugha moja (mame –Kiswahili)zama hizo zikibadilika kuwa lahaja za maeneo tofauti.Baada ya lahaja hizo kugawanika katika makundi mbali mbali kama vile lahaja za kaskazini na kusini (Massamba, 2007). Kuhusu lahaja ya Kipemba, pia mgawanyiko ulijitokeza baina ya Kaskazini na Kusini. Baada ya mwachano, lahaja ya Kipemba ikagawanyika makundi mawili, yaani Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Lahaja hizi zikaanza kutofautiana kwa baadhi ya msamiati kutokana na

sababu kwamba zimekwisha ingiza msamiati na usemaji mwingi wa kimazingira mapya kutokana na tofauti ndogo za historia mpya.

Kulingana na data yetu ya utafiti kuna tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha kaskazini na Kusini zitokanazo na sababu ya kihistoria. Tofauti hizi hujibainisha katika matamshi na baadhi ya msamiati. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.11: Sababu za Kihistoria

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
mvyele	*nzee*	‘mzee’
mvyazi	*nzazi*	‘mzazi’
mwanamwali	*mwari*	‘mwanamwari’
nshikyana	*nsichana*	‘msichana’
mvulyana	*mvulana*	‘mvulana’

Kupitia mifano katika jedwali hapo juu linatudhihirishia kuwa kuna tofauti za kimsamiati kutokana na sababu za kihistoria. Hata hivyo, tofauti hizo sio kubwa sana kutokana na kuwa lahaja hizi zina uhusiano wa awali kihistoria. Hivyo kwa mujibu wa data yetu sababu hii ilionesha kwa jumla ya maneno 14 kati ya maneno 143 sawa na asilimia 10% yanaonesha sababu ya tofauti msamiati inayotokana na sababu ya kihistoria.

4.5.3 Kutawanyika kwa Watu

Kimsingi inadaiwa kwamba lahaja za Kiswahili ni lugha zenye chimbuko moja ambazo zimepata kuachana na kugawanyika na kuwa lahaja (Massamba, 2007). Kisha kutokana na mijongeo ya watu mbalimbali, mitagusano yao ambayo inatokana

na kuachana kwao, watu hao huanza kutofautiana kimatamshi na msamiati usio wa msingi. Kutokana na mwachano wa muda mrefu baadhi msamiati hutofautiana kabisa. Tuangalie mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 4.12: Mtawanyiko wa Watu

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
komo	bingu	‘komo’
Tilifu	angamia	‘angamia’
Zidiwa	chachiwa	‘zidiwa’
Cheleya	shuka	‘shuka’
Himiza	faulisha	‘himiza’

Kutokana na mifano katika hapo juu tunaona tofauti za kimsamiati zinazosababishwa na watu wa Kaskazini na Kusini kutawanyika katika mielekeo tofauti. Katika sababu hii watu wa Kaskazini wametawanyika katika maeneo mbalimbali ya kaskazini na watu wa kusini wametawanyika katika maeneo mbalimbali ya kusini. Mtawanyiko huu umepeleke tofauti za kimsamiati kama tulivyoona hapo juu.kutokana na data yetu sabadu hii iaoneshwa kwa jumla ya maneno 26 kati ya143 sawa na asilimia 37% yanaonesha sababu ya tofauti ya msamiati inayotokana na mtawanyiko wa watu.

4.5.4 Shughuli za Kiuchumi

Shughuli za kiuchumi pia, zinatofautisha msamiati wa lugha kutokana na shuguli kuu za kiuchumi za sehemu hiyo. Kwa mfano jamii inayohamia karibu na vyanzo vya maji hujishughulisha na uvuvi wakati jamii inayohamia sehemu isiyo na vyanzo vya maji huweza kujishughulisha na kazi kama vile kilimo, ufugaji, uhunzi ambapo shughuli hizi huathiri lugha inayozungumzwa na wazungumzaji kwa sababu

huzalishwa maneno yanayoendana na mazingira yanayohusika. Mfano watu wanaojishughulishana uwindaji wanatofautiana kimsamiati na wanaojishughulisha na uvuvi katika baadhi ya maneno.

Hivyo basi, kutokana na sababu za shughuli za kijamii hutofautiana kwa baadhi ya sauti za msamiati. Msamiati huu mpya ndio hupelekea tofauti za kiusemaji baina ya lahaja moja na nyingine. Tuangalie mifano hapa chini:

Jedwali Na. 4.13: Sababu za Kiuchumi

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
pwaa	*pyaa*	‘bahari’
liko	*diko*	Bandari
vuwa	*vuya*	‘vua’
lema	*dema*	‘dema’
dau	*ntumbwi*	‘mtumbwi’

Mifano katika jedwali hapo juu inadhihirisha kuwa kuna tofauti za msamiati baina za Kipemba cha kaskazini na kusini zinazosababishwa na shughuli za kiuchumi. Katika mifano hiyo, maneno ya Kaskazini yametofautiana na maneno ya kusini kwa baadhi ya sauti za kimatamshi. Hivyo kwa mujibu wa data yetu maneno 19 kati ya 143 sawa na asilimia 13 % yanaonyesha sababu ya tofauti ya msamiati inayotokana na shughuli za kiuchumi za jamii.

4.5.5 Mwingiliano na Jamiilugha Nyingine

Kwa mujibu wa Massamba (2007) jamiilugha mbili ambazo zina mnasaba yaani zenye kutokana na mame-lugha moja huathiriana zaidi kuliko zile ambazo ziko mbali kidogo. Kutokana na sababu za mwingiliano wa watu wenye tamaduni tofauti hupelekea watu wa sehemu moja kutofautiana na watu wa sehemu nyingine kimsamiati. Kwa mfano watu wa Kaskazini wanamaingiliano ya karibu na lahaja za Kenya kama vile Kibajuni, Kiamu, Kipate na Kikichaka. Watu wa kusini wana maingiliano na watu wa kusini yao kama vile Watumbatu na Wamakundichi.

Hivyo basi, jamii ya watu inapohamia katika mazingira mapya hukutana na mambo mapya. Msamiati huu mpya ndio hupelekea tofauti za kiusemaji baina ya lahaja moja na nyingine. Tuangalie mifano hapa chini:

Jedwali Na. 4.14: Sababu za Mwingiliano

Kaskazini	**Kusini**	**Tafsiri**
nchamo	*bacha*	‘mkeka mkongwe’
lepe	*bangwe*	‘kuhisi usingizi’
gunda	*dundu*	‘baragumu’
asiza	*asa*	‘achiza’
vova	*boba*	baribika

Kutoka na mifano hapo juu tunabaini kuwa kuna tofauti za kimsamiati zitokanazo na mtawanyiko wa watu kutokana na mtawanyiko huo watu wa Kaskazini wana ujirani wa karibu na lahaja za Kaskazini kama vile kibajuni, Kiamu na Kipate. Kwa sababu maneno kama vile lepe na gunda yanapatikana pia katika lahaja ya Kibajuni. Kwa

upande wa kipemba cha kusini, lahaja hii ina uhusiano wa karibu na lahaja ya Kitumbatu. Kwa mfano, bangwe, asa na boba yanapatikana katika lahaja ya Kitumbatu.

Hivyo basi kwa mujibu wa data yetu sababu hii inaoneshwa kwa jumla ya maneno 20 kati ya maneno 143 sawa na asilimia 14% yanaonyesha sababu ya tofauti ya msamiati inayotokana na mwingiliano wa jamii lugha nyengine.

Hata hivyo Kipemba cha kaskazini na Kusini kuna msamiati mwingi unaofanana baina yao pia na kiswahili sanifu, ambapo tofauti ni ndogo tu katika baadhi tu ya msamiati huo,.Kiwango kikubwa cha tofauti za msamiati kinatokana na tofauti za kimatamshi. Hii ni kwa sababu lahaja hizi zinatokana na mame lugha moja,kwa hiyo lugha zenye asili maja huachana kwa baadhi tu ya matamshi na msamiati usio wa msingi.

4.6 Muhutasari wa Sura

Katika sehemu hii tumebainisha na kujadili tofauti za kimsamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Tofauti hizo zimejibainisha katika viwango vya kifonolojia (sauti), kimofolojia na kileksika. Katika kiwango cha kifonolojia tumeangalia msamiati wa Kaskazini unavyotofautiana na ule wa Kusini kutokana na mpishano wa konsonanti, mpishano wa irabu, mpishano wa nusu-irabu, udondoshaji wa sauti, ukaakaishaji, lafudhi, mpumuo na kibenua ulimi. Aidha, tumeonesha tofauti za msamiati kileksika yaani maneno yanavyotofautiana kimaumbo ingawa yana maana sawa. Mwisho tumeelezea sababu zinazopelekea tofauti za kimsamiati baina ya

Kipemba cha Kaskazini na Kusini .Sababu hizo ni pamoja na Umbali wa maeneo kijografia ,kihistoria,kutawanyika kwa watu,shughuli za kiuchumia na Mwingiliano wa jamii lugha nyengine.

SURA YA TANO

MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza vipengele kama vile muhutasari wa mjadala, kujibu maswali ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2 Muhutasari wa Mjadala wa Utafiti

5.2.1 Muhutasari wa Jumla

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini, lahaja ambayo inazungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Utafiti huu umekusudia kufikia malengo mahususi mawili. Lengo la kwanza, kubainisha tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Pili, kuelezea sababu zilizopelekea tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini.

Ubainishaji wa tofauti za msamiati na mjadala wake umefanyika kwa kutumia nadharia ya ***Isimulinganishi***. Nadharia hii imetumika ili kulinganisha na kulinganua msamiati wa Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Ili kuibua tofauti hizo za msamiati, vigezo vitatu vya mbinu linganishi vimetumika kuchambua matini zilizokusanywa uwandani. Kigezo cha kwanza ni kuchunguza kukubaliana kwa sauti katika maneno. Kupitia kigezo hiki tumeweza kulinganisha sauti za msamiati wa Kaskazini na Kusini ili kuona kwa kiasi gani unafanana na kutofautiana. Kigezo cha pili ni

kuchunguza msamiati wa msingi. Kigezo hiki kimetumika kuchunguza msamiati unaohusu vitu vya kawaida katika mazingira ya wasemaji wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Vitu vilivyo vya asili katika mazingira haya, majina ya viungo vya mwili na shughuli za kila siku za jamii vimechunguzwa. Kigezo cha tatu ni kuchunguza maumbo ya maneno ili kuona kama lahaja hii ina maneno yenye maana moja lakini yana maumbo tofauti. Maneno yanayotofautiana kimaumbo lakini yakiwa na maana sawa.

Kupitia vigezo hivyo vya isimulinganishi hatimaye tumeweza kubainisha, kuelezea na kujadili tofauti za msamiati baina ya lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Nadharia hii ni faafu kwa kulinganisha lugha au lahaja mbili zenye mnasaba yaani zinazotokea kwenye mame-lugha moja.

5.2.2 Muhutasari wa Ugunduzi

Katika mchakato wa kubainisha, kueleza na kujadili tofauti za kimsamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini, pia tulijielekeza kujibu maswali ya utafiti (taz. § 1.5) ambayo msingi wake ni malengo mahususi ya utafiti (taz. § 1.4.2). Maswali hayo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza lilikuwa: *Kuna tofauti gani za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini?* Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa kuna tofauti kadhaa za msamiati zinazojitokeza baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Miongoni mwa tofauti hizo za msamiati ni tofauti za kimatamshi au kifonolojia, kimofolojia na kileksika, Tofauti hizi tumezibainisha na kuzijadili kwa kina § 4.2 hadi 4.4 katika tasinifu hii.

Kwa hivyo tumebaini kuwa kuna muachano mkubwa wa msamiati kifonolojia baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Aidha, kwa baadhi ya maneno tofauti hizi pia zinaachana na Kiswahili sanifu.

Swali la pili lilikuwa: *Ni sababu zipi zilizopelekea tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini?* Majibu ya swali hili yameelezwa kwa kina katika § 4.5 hadi 4.6 katika tasinifu hii. Kuna sababu kadhaa zilizobainishwa na watoa taarifa wakati wa mchakato wa ukusanyaji wa data. Kwa mujibu wa utafiti kuna sababu kama vile mwachano wa watu kijiografia, makundi ya watu katika jamii, tofauti za shughuli za kiuchimi, kipato, elimu na kadhalika. Sababu nyingine ni maingiliano ya watu mbalimbali, kuhamahama, na nyinginezo.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu umejaribu kutoa maoni ya awali kuhusu tofauti za msamiati wa lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini katika kisiwa cha Pemba. Tumeona kuwa kuna tofauti za msamiati baina ya Kaskazini na Kusini. Aidha, ingawa kwa hakika kuna tofauti za kimsamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini ambazo pia zinatofautiana na Kiswahili sanifu kuna mambo kadhaa tunaweza kujiuliza.

Swali la kujiuliza ni; kwa nini Kipemba kizungumzwacho Kaskazini kinatofautiana kwa kiasi kikubwa na Kipemba cha Kusini na pia Kiswahili sanifu? Kwa mwelekeo huo, je katika kisiwa cha Pemba kuna lahaja zaidi ya moja? Kwa kuwa tumeshasema kuwa utafiti wa kina unahitajika zaidi, maswali hayo hayahitaji majibu ya harakaharaka. Tunataraji kwamba utafiti wa kina zaidi utabainisha tofauti nyingine

zaidi za kimsamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini. Kwa hivyo, tunategemea kwamba utafiti huu utawafanya watu wengine waanze kuchunguza kwa kina zaidi tofauti kuhusu asili na chimbuko la Kipemba cha Kaskazini na kile cha Kusini. Uchunguzi wa chimbuko utasaidia kugundua asili ya lahaja ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini.

5.4 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti Zaidi

Si jambo jepesi kwamba utafiti kwa mara moja unaweza kujitosheleza na kudaiwa kuwa umemaliza kila kitu katika eneo ulilolichunguza. Kwa hivyo ni kweli kwamba utafiti huu haujakamilisha kila kitu. Tunaweza kuuchukulia kuwa ni hatua ya awali ya kupambanua tofauti za msamiati baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini katika kisiwa cha Pemba. Hivyo basi, tunapendekeza kwamba vipengele vingi zaidi vya kiisimu kama vile, fonolojia, mofolojia, miundo nk vinahitaji kuchunguzwa kwa kulinganisha na kulinganua lahaja za maeneo haya. Mada tunazozipendekeza ni pamoja na asili na chimbuko la Kipemba cha Kaskazini na Kipemba cha Kusini. Pia kunahitajika utafiti wa kulinganisha lahaja za maeneo mbalimbali ya vijijini katika Kisiwa cha Pemba.

MAREJELEO

Adam, J & Kamuzoro, F (2008). *Research Methods for Business and Social Studies* Morogoro, Mzumbe Book Project

Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. New York. Macmillan Publishing Co. Inc.

Ash & Boberg (2006). Southern Dialect Report.en Wikipedia.org /wiki/southern-American English.

Ashton, E. (1944) *Swahili Grammar*. London. Longaman.

Bakar, M. (1981). *"Uchunguzi wa Lahaja za Kiswahili"*. (Makala ya Semina). Zanzibar.

_____ (1985). *The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects*.Dietrich Reimer Verlag,Berlin

Batibo, H. M (1981). "*The Sothern Swahili Dialects*". (Makala ya Semina). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_____ (1982). "*Mawazo ya Mwanzo kuhusu Uhusiano wa Lahaja za Kiswahili za Kusini"* (Makala ya Semina). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Campbell, L. (2004). *Historical Linguistics: An Introducation*. (chapa ya 2) Cambridge. The MIT Press.

Cohen, L, L. Manion na K. Morrison (2000). *Research Methods in Education*. Toleo la 5. London: Rutledge Falmer.

Cooper, Robert (1989). *Language Planning and Social Change Cambridge*: Cambridge University Press.

Ingrams, W. H (1924). “The Dialects of the Zanzibar Sultanate” in Bulletin of the School of Oriental and African Studies, Vol.III, Part III, London, pp 533-550.

_____ (1931). “Zanzibar Notes on the Dialects”, iliyowasilishwa London CASS (1967).

Gesare, H. L (1992). A Morphological Typological of Ekegusii in Structural Frame Work. M.A Thesis (Haijachapishwa), University of Nairobi Kenya.

Juma, H. Kh (2011). “Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na cha Wete katika Kisiwa cha Pemba”. Tasnifu ya M.A Kiswahili (haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Khamis, S. A. M (1984). “Urban Versus Rural Swahili: A Study of Pemba Varieties”. (Tasnifu ya Uzamivu, Haijachapishwa) Leipzing: Karl Marx University.

Kihore, Y. M, D. P. B. Massamba na Y. P. Msanjila (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA): Secondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kipacha, A. (2004). *Lahaja za Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria. Dar es Salaam: KIUTA.

Kothari, C. R (1990). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern.

_____ (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P).

Lambert, H.E. (1957). *Ki-Vumba: A Dialect of Mombasa Coast.* Kampala. East African Swahili Commettee.

_____ (1958a). *Chi-Chifundi: A Dialect of the Southern Swahili Coast*. Kampala: East African Swahili Commettee.

_____ (1958b). *Chi-Jomvu and Ki-Ngare: Sub-dialects of the Mombasa Area*. Kampala. East African Swahili Commettee.

Maganga, C. (1991). "*A Study of the Morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Makunduchi".* (Tasnifu ya uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Masebo, J. A & Nyangwine N., (2002). *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili: Kidato cha tano na sita*. Afroplus Industries Ltd. Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B (1987). "*The Effects of Language Modernization on the Phonological System of the Kiswahili Language".*ktk. KISWAHILI: Journal of the Institute of Kiswahili Research. Vol. 54/1 & 2.IKR. Dar es Salaam.

_____ (1994). *"Historia ya Kiswahili"*.ktk. Kijarida cha CHAKA. Na. 1:34-41. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_____(2002). *Historia ya Kiswahili*: 50BK hadi 1500BK. Nairobi: JomozKenyatta Foundation.

_____ (2004). *Kamusi Ya Isimu Na Falsafa ya Lugha*. Dar es salaam. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es salaa

_____ (2006). "*Kiswahili cha Musoma Mwanzo wa Lahaja Nyingine?*" ktk KISWAHILI: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mgullu, R. S. (2001). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Longhorn Publishers. Nairobi.

Mshindo, H. B (1989) . "*The Use of KA in Pemba Swahili Variety*". (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa). University of Dar es Salaam.

Nurse, D (1982). "*A Tentative Classification of Primary Dialects of Swahili"* ktk. Sprache und Geschichte in Afrika. Vol. 4, Hamburg,

Nurse, D & Hinnebusch, T. J (1993). *Swahili and Sabaki*. Califonia: Califonia University.

Nyandago, F. O (2013). *Uchanganuzi Linganishi wa Sintaksia ya Sentensi Sharti ya Kiswahili Sanifu na Ekegusii*. Chuo Kikuu Nairobi Kenya.

Nurse, D na Spear, T (1985). *The Kiswahili*: Reconstructing the History.gggg

Polome, E. C (1967). *Swahili Language Handbook*, Center of Applied Linguistics, Washington DC.

Prasad, T (2012). *Acouse in Linguistics*. PHI Learning Private Limited. New Delhi

Saucleux, C. (1909). *Grammaire des Dialectes Swahili Language.*Cambridge.

Stigand, C. H (1915). *Grammar of Dialect Changes in the Swahili Language*. Cambridge University Press.

Sture, J. (2010). *Ethics in Research Project*: Some Guidance on Recognising and Addressing Ethical Issues: University of Bradford; UK.

Temu, C. (1980). *"Lahaja za Kiswahili".* Ripoti ya Utafiti, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Whiteley, W. H. (1956). *KIMTANG'ATA: A Dialect of Mrima Coast – Tanganyika*. Kampala: East African Swahili Committee.

VIAMBATISHO

Kiambatishi I: Dodoso la Kuchunguza Tofauti ya Msamiati

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

DODOSO ZA KUCHUNGUZA TOFAUTI ZA MSAMIATI BAINA YA LAHAJA YA KIPEMBA CHA KASKAZINI NA KUSINI

Maelezo:

- Baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu yana vibadala ambavyo hutumiwa maneno mengine. vibadala hivyo vina maana sawa au inayokaribiana na maneno hayo.

-Tafadhali andika istilahi au maneno mbadala ya maneno yafuatayo kulingana na yanavyotumiwa na watumiaji a luhga ya Kiswahili wa eneo unaloishi.

asubuhi……

ambalo…….

angalia…….

aibu ……

beba …….

birika…….

bandari……

chama……

chumvi……

chicha…….

chupia…….

chungu……

choo……

dagaa……

d afu …….

desturi……..

dema……..

elekeza……..

eleka…….

egemea…….

egesho ……

Finya……

Faraja……

funza …….

funguo……

gudulia…….....

ghadhabu……

genge ……..

Gusa……..

haribika…….

hofu……

huzuni……..

hamaki…….

himiza …….....

inga…….

iba……..

Inda……..

Jasiri……

Jamba…….

Janga……..

Jua…….

Jiwe……

Kiambaza…….

Kanyaga…….

Kata…….

Kwenda……

Labda……

Lenga……

Lima……

Lulu……

Mwambie…….

Mrama……

Mrefu…….

Mvua……

Mtumbwi……

Ndege……

Nenda……

Nyonda……

Nyongeza……..

Neema……

Nakama……

Nuna……

Ondoa……

Ozesha……

Okota……

Pumua……

Potea……

Poteza……

Pona……

Pachua…….

Ramli……

Rambuza……

Roa……

Rusha……

sengenya……

shelisheli……

shika…….

sulubu……

sukutua……..

tahiri……..

tambara……..

tapika…….

teleka……

toka……..

uzia……..

ugua……

utomvu…….

vizia……

vumbi…….

vuna……

wakala……

wakati……

wema……

wao……..

yaya……

yowe…….

yungiyungi…….

zingizi……

zidiwa……

Kiambatishi II: Mwongozo wa Maswali ya Hojaji

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

Maswali ya Hojaji ya Kuchunguza Tofauti za Msamiati Baina ya Kipemba cha Kaskazini na Kusini

Hojaji hii inalenga kukusanya taarifa za tofauti za kimsamiati baina Kipemba cha Kaskazini na Kusini kama unavyofahamu na kutumia lugha inayohusika. Majibu yatakuwa siri kati ya mtafiti na mtafitiwa. Sio lazima kuandika jina lako katika hojaji hii.

SEHEMU A

1.JINSI ME [ ] KE [ ]

2.UMRI i)75-50 [ ] ii)49-25[ ] iii)24-15 [ ]

3.Kiwango cha elimu: i)Elimu ya msingi [ ],ii)Elimu ya sekondari [ ],iii)Diploma [ ]

iv)Shahada [ ] v) Uzamivu [ ] v) Sikusoma [ ].

4.Kazi yako …….

5.Cheo chako……

SEHEMU B:KUBAINISHA TOFAUTI ZA KIMSAMIATI.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kulingana na maelekezo husika.

6.Je,kuna tofauti zozote zinazojidhihirisha katika uzungumzaji wa Kipemba cha kaskazini na kusini,weka alama ya vema kadri ya ufahamu wako.

Ndio [ ] Hapana [ ].

7.Kama ndio ni tofauti za kimsamiati [ ], kimuundo [ ], kimatamshi [ ].

8.Tafadhali taja maneno unayoyatumia ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu

NENOKILUGHA	KISWAHILI SANIFU
i)……..	……
ii)…….	……
iii)……	……
iv)……	……..

Kiambatishi III: Orodha ya Msamiati Uliobainishwa na Watafitiwa kwa Kutumia Dodoso

KISWAHILI SANIFU	KASKAZINI	KUSINI
asubuhi	unju	usubuhi
ambalo	ambalyo	velo
angalia	chunza	ola
aibu	fedheha	tahayuri
beba	eleka	kweleka
birika	birika	bilika
bandari	likoni	dikoni
chama	kyama	chama
chumvi	shumvi	chumvi
chungu	kyungu	chungu
choo	kyoo	choo
dagaa	dagaa	dagaya
dema	lema	dema
finya	fikicha	bigija
funza	funza	fuza
funguo	funguo	funguyo
genge	genge	kipesa
inga	inga	winga
jiwe	iwe	jibwe
kiambaza	kiza	kiwamba
kanyaga	uwata	banja
labda	rabuda	rabda
lenga	gea	tupa
mwambiye	mwambile	mwambie
mrefu	nnrefu	nrefu
mtumbwi	dau	mtumbwi
mvua	mvua	vua
ndege	repuleni	zepuleni
nenda	nende	nde
ondosha	usha	yusha
ozesha	oza	yoza
okota	okoto	yokoto
potea	geleka	aga
pona	besa	poa
pacha	dengua	pachua
sengenya	amba	sengenya
shelisheli	shelisheli	Sheli/mbobo
sukutua	chukuchua	sukutua
tapika	kovyoka	govyoka
toka	awa	yawa
vizia	doeya	nyemelea

vumbi	vumbi	dumbi
wakati	ukati	wakati
wao	wao	veo

Kiambatishi IV: Orodha ya Msamiati Uliotafitiwa

Kipemba cha Kaskazini	**Kipemba cha Kusini**	**Kiswahili sanifu**
Asiza	*Asa*	Zuia mtoto kunyonya
Boshori	*Kofia*	Kofia
Cha	*Ogopa*	Woga
Cheleya	*Shuka*	Shuka
Doweya	*Nyemeleya*	Vizia
Funguo	*Funguyo*	Funguo
Funza	*Fuza*	Funza
Gosa	*Koleza*	Koka (moto)
Gowe	*Vita*	Vita
Gunda	*Dundu*	Baragumu
Hakifai	*Uzanya*	Kisichomaana
Himiza	*Faulisha*	Himiza
Kama	*Ja*	Kama
Kamange	*Kayamange*	Kamange
Kibago	*Kigoda*	Kigoda
Kidinya	*Kidigi*	Kidogo
Kidudu	*Mdeke*	Uume wa mtoto
Kidiri	*Cheza*	Weza
Kiza	*Kiwamba*	Ukuta
Kiza	*Kiwamba*	Kiambaza
Kumiza	*Beza*	Beza

Kipemba cha Kaskazini	**Kipemba cha Kusini**	**Kiswahili sanifu**
Kunguwaa	*Kwaa*	Jikwaa
Kupakasa	*Kusuka*	Kusuka (ukili)
Kuvalia	*Saura*	Kuvalia
Lepe	*Bangwe*	Kuhisi usingizi
Machaza	*Wali*	Wali
Mimba	*Tumbo*	Tumbo
Mvi	*Jaje*	Vipi
Penjewa	*Shaga*	Furahi
Sasanya	*Funganya*	Kusanya
Shombwe	*Rikicha*	Vumba
Songa	*Suka*	Suka (nywele)
Ta	*Taga*	Taga
Teleka	*Injika*	Teleka
Tilifu	*Angamia*	Angamia
Totovu	*Bunju*	Bunju
Tumbwija	*Bavi*	Lengelenge
Tumbwi	*Daka*	Dafu Changa
Ukati	*Wakati*	Wakati
Ulimbo	*Udande*	Urimbo
Ungwe	*Kamba*	Kamba
Uteu	*Ungo*	Ungo
Uwata	*Banja*	Kanyaga

Kipemba cha Kaskazini	**Kipemba cha Kusini**	**Kiswahili sanifu**
Vua	*Vuya*	Vua
Vihibi	*Chochoma*	Kichache
Vina	*Hangaika*	Hangaika
Vova	*Boba*	‘Haribika’
Wao	*Veo*	Wao
Yeye	*Vee*	Yeye
Yupo	*Kaapo*	Yupo
Mudi	Toyeza	Weza
Dabwe	*Magwa*	Magwa
Igi	*Yai*	Yai
Labuda	*Rabda*	Labda
Majani	*Magani*	Majani
Mwendawazimu	*Mbole*	Mpumbavu
Chapa	*Kutota*	Nguo ilioroa
Dengua	*Pachua*	Pachua
Tumbi	*Pakacha*	Pakacha
Nndu	*Panga*	Panga (kifaa)
Papai	*Bokwa*	Papai
Pengine	*Keje/keli*	Pengine
Wana	*Butana*	Pigana
Gurubi	*Gubi*	Gubi
Besa	*Poa*	Pona

Kipemba cha Kaskazini	**Kipemba cha Kusini**	**Kiswahili sanifu**
Wayo	*Wayowayo*	Wayo
vuga	*buga*	Sumbua
Sheli	*Shelisheli*	Shelisheli
Chukuchua	*Sukutua*	Sukutua
shonya	*bonya*	sonya
Uteu	*Ungo*	Ungo
Kibiya	*Tanu*	Mkungu
Chunza	*Ola*	Angalia
Unju	*Usubuhi*	Asubuhi
Bofya	*Bonyeza*	Bonyeza
Pwaga	*Chemka*	Chemka
Poshi	*Chii*	Chini
Kyombo	*Chombo*	Chombo
Chukua	*Twaa*	Chukua
Tutu	*Chunusi*	Chunusi
Omeka	*Tuwa*	Eka
Enza	*Fata*	Fuata
Penjewa	*Mshango*	Furaha
Genge	*Kipesa*	Genge
Hadhabu	*Hamaki*	Ghadhabu
Pande	*Gogo*	Gogo
Haraka	*Upesi/hima*	Haraka

Kipemba cha Kaskazini	**Kipemba cha Kusini**	**Kiswahili sanifu**
Tegua	*Epua*	Epua
chepeu	*chepeyu*	chepeu
kyeupe	*cheupe*	cheupe
kyakwe	*chake*	chake
nndefu	*nrefu*	mrefu
nndisho	*nrisho*	mrisho
kamange	*kayamange*	kamange
gurubi	*gubi*	gubi
boko	*bokoboko*	bokoboko
shushuka	*chuchuka*	kua
zeme	*veme*	zeme
puma	*poma*	pumua

Kiambatishi III: Matini Mbalimbali

Matini 1 : MAZUNGUMZO YA WAVUVI KIIJIJI CHA MWAMBE

MT1**:** Bwan Juma kumwono uyule kayamange?

MT2: Kayamange n yupi mwamme?

MT1: Si uyule mwana wa nzee Pandu.... kawa kayamange.

MT2: Ha ha haa ama mwamme kuwa mbishi... kibera uyule kawa kayamange?

MT1: Enhe... kanibili wayowayo wangu... hambigija magubi taa.

MT2: Miye sijaona kayamange apale... ungeuwa mwana wa watu....

Matini 2: MAZUNGUMZO BAINA YA WAZAZI NA WATOTO

Baba: nyie wana mwacherewa

Mama: e kwani mwe waa?

Mtoto: Twe kule kwa bankuu

Mama: Kwe na ni?

Mtoto: Tunkwenda zinga vishuka!

Baba: Ha basi fanyani muawe

Mtoto: namba mtandiyo wangu siuwono

Baba: awa... awa utenda ivyo ivyo maana weye ntoto weye umviya.

Matini 3: VIJANA KATIKA MCHEZO WA MPIRA

A: nchunze uyo Mfaki yuwamfunda mwinziwe kwa maguu tu

B: Ejama pasitakewana siye twajuwa n’goli ilyo.

C: Ha mbona pya nyosi mwanikaliya miye? Weye kaa goliniko

B: Muache kama hebu kaa kipa t^{h}akaa miye

C: Hatwebu hukidiri jambo utatufungesa.

A: Haya! Bahamadi kashachukiwa. Bakar wajangiya weye?

Matini 4: MAZUNGUMZO YA MJUKUU NA BIBI YAKE KANGANI

Mjukuu: Bibi shikamoo.

Bibi: Marahaba habari za nyumbani, babu kunanigeya hunipitili.

Mjukuu: He! Bibi we nehiumwa na dicho ujiti hewegota kiini cha dicho ela umangiya sehemu hii nenda sipitalinimarudi nimavungwa dawa. Hapo nsahavunguliwa basi huona kana nnaetiwa moto ndani ya dicho, sasa hapo sivyeza tena wala mwanga siuolo watu wamanidaukiya hali ndo ja hiyo sekugeya bibi.

Bibi: Basi miye huu nguu ulikuwa unyoroko tu, ukaa ja kisiki.

Mjukuu: Hukunjuliwa wakaukanda kwa maji moto na magani ya mbono?

Bibi: Ta sefika iko huchukuliwa hivi ukajishwa hivi ukaachiliwa uwa vilevile, akaja iyo njombayo ibakili yakwe zamu akasema endeswe sipitali Nkoani, tena hendeswa Nkoani hamuola Nchina anavyochachawika akaudosadosa apofika hapa babu, kaji na nsumari upata ja hapa ama eutila woti.

Mjukuu: Kautii sehemu gani?

Bibi: Pajani nanguruma babu apokwisha ukenda nkasi mpaka upokoma nsumari.

Mjukuu: Alikupiga shindano ya gazi ati kwaza.

Bibi: Henipiga Walahi nipata uperesheni mbaa hawa sina akili babu lada ndo uvimbe ela heletuna guu. Lakini lishaaza kuchuruza saha kumavitambuwa tena hatiwa

chepe mbili ele guu linyoroko vilevile. Weketwa watu sina habari kama kumaja watu guu limakacha iketwa gari hajiswa nyumbani.

Matini 5: MAZUNGUMZO YA MAKAME NA PANDU CHOKOCHO

Makame: Mzee Pandu wenga vipi?

Pandu: Kwani?

Makame: Naona jana nimenda shamba nikiola huku kumalyo hitizama huku kumalyo mpunga wo pya umaharibiwa n ndudu.

Pandu: Uyu njukuu wangu mosi izi kananichagiza, kananifuata shamba. Miye mmakaa sina habari katakwenda kwenye kile kijito katangiya.

Makame: Tena kufanya maarifa gani?

Pandu: Nimvutu.

Makame: Kumvutu vi? Mana maji yale kumasimama?

Pandu: Maji mangi simi ela engia uku nsha nsha, angengiya katikati kingekugwa kisindo miye mmapiga kikelele kuntowa huku ndudu wanaharibu. Bahati zuri wakaawiya watu wakanisaidiya watoto wa leyo watukutu. Sasa mmakoma kunchukuwa tena kuja nipa kutajasikila mmachomoka wanga.

Matini 6: MZEE ANAHADITHIA MWAKA WA NJAA

Ama mwaka sabiini na mbili kwengiya njaa taa nshi ikinuka baruti, maana kwena ukame juwa kali vyakulya pya vyekauka, ela Muungu eleta baraka ya samaki ama ukenda pwani ukyezagwiya samaki ta ukawaacha.

Watu wekiponeya samaki na nazi ama nazi zeeko nazo zikigwa umo minazini lakini watoto la wakifa kwa njaa. Watu wekiawa apa wakenda ta N'gogoni Kwale, Makangale na Tondooni wenda chimba ushoshoni na ndinga, ta yekuwa watu wangine hawakikubali tena kuchimbiwa mashambani mwawo mwaka uwo ndiwo palipozuka steti Nkandaa, watu wakitoka hapa wakenda Tanga, Mambasa wakija na michele na dona ela ndiyo ye magendo ukigwiwa wenda laliya maviyo jela. Shumba zikingiya mashuwa kama nini ela kwena sikyuriti mmoja akiitwa Kibaka akenda akyoteya akigwiya watu, naye kwawo kwe ukouko Kiuyumbuyuni, kuchwa akitiay watu mbiyoni. Ama ta kilipokwisha kibope hicho tutaabani twaolewa roho.

Matini ya 7: WANAWAKE WA KIUYU MBUYUNI

Maisha yetu siye watuwake apa Kiuyu nzima twaokolewa mmwani. Kusema kweli mwani watuokowa maana hawo waume wetu siye si wachumi vyema, wawo n'wakwendavyawo ago kuchwa wanjiani, hutubwaga siye na watoto apa wataka kulya wataka vaa kama huna ta nshikizo mmauti. Kazi ya mwani ni ngumu ela si sana, ugumuwe hasa ukati waanza sasa maana hadi uzinge pegi ukaziike shamba ukafunge taitai ukazifunge kwa majiti ukimaliza utaabani, miye hiondoka apa asubuhi siku nyingine narudi mangaaribi ya usiku. Mwaka jana miye nevuna hiuza hipata zawadi hikatia wanagu nguwo za sikukuu maana mwani wangu mwingi miye ni kotoni kuliko sipisamu, na kotoni m'bora beyi. Alihamdullilahi twapata ela beyi ike ndigi twawaomba matajiri watwongezee.

Kiambatishi IVI: Barua ya Ruhusa ya Utafiti

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

FACULT OF ARTS AND SOCIAL SCIENCES

P.O. Box 23409
Dar es Salaam, Tanzania
http://www.openuniversity.ac.tz

Tel: 255-22-2666752/2668445
ext.2101
Fax: 255-22-2668759

22/5/2015

DIRECTOR,

DRPS,

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA,

P.O. BOX 23409,

DAR ES SALAAM

Dear Sir,

Re: CLEARANCE TO CONDUCT RESEARCH WORK FOR, ALI SITI FAKI

This is to inform you that, ALI SITI FAKI is an M.A student under my supervision.

Title of the research proposal: TOFAUTI YA MSAMIATI WA LAHAJA KIPEMBA CHA KASKAZINI NA KUSINI. **Registration No:** PG201401860

I am writing to certify that, the student's proposal is ready to my satisfaction and she can proceed with data collection.

I therefore, recommend her to you to be granted research clearance for data collection in the field from **23/5 -5/6, 2015**. The field will be done in **micheweni and Mkoani district at the fallowing shehias.**

Micheweni- Maziwangombe,kiyuyu and Micheweni

Mkoani - Mwambe,kangani and chokocho. Theletter is to be addressed to :

D C **Micheweni- JABU KHAMIS MBWANA**

D C Mkoani –HEMED SULEIMAN ALI .

Thank you in advance.

Sincerely,

Dr. Zelda Elisifa

Lecturer in Linguistics and Literary Studies

Supervisor